# Nipashe

Ijumaa Aprili 24, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580214

www.ippmedia.com

The Guardian digital | nipasheTZ | nipasheTZ | nipasheTZ | 0745 700710




## TOLEO MAALUM

## Dk. Reginald Mengi alipenda kuiendeleza sekta ya habari

UK. 3




UKURASA 14

## TISHIO CORONA

# DC aanika kilichojiri Hospitali ya Amana

**NI** hofu ya wagonjwa kutoroka, Polisi wachunguza, Waziri aonya watoa huduma kukimbia wagonjwa...

*Endelea ukurasa 2*



Waombolezaji wakiwa katika mazishi ya Mbunge wa Kuteuliwa, Mchungaji Dk. Getrude Rwakatare yaliyofanyika katika Kanisa la Mlima wa Moto Mikocheni 'B', jijini Dar es Salaam jana. Picha ndogo chini kulia: Jeneza lenye mwili. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**.

## BAA LA CORONA



Matunda na mboga ni vyakula muhimu katika kuongeza kinga ya mwili hasa kipindi hiki cha mlipuko wa ugonjwa wa Covid - 19. Kabla ya kula unashauriwa kusafisha mikono yako vizuri kwa maji tiririka na sabuni kisha osha vyakula hivyo kwa maji safi, hasa vinavyoliwa bila kupikwa.

WHO

- Epuka mikusanyiko ya watu
- Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka
- Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana
- Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo

## JELA MAISHA KWA KUBAKA BINAMU YAKE WA MIAKA 8

UKURASA 9

# Serikali yataja bei ya sukari

UKURASA 2




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play | App Store


MICHEZO — YANGA SASA KIMYA KIMYA UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

# DC aanika kilichojiri Hospitali ya Amana

**Na Waandishi Wetu**

MKUU wa Wilaya ya Ilala, Sophia Mjema (pichani), ametoa ufafanuzi kuhusu taarifa za wagonjwa waliothibitika kuwa na virusi vya corona waliokuwa wamelazwa katika Hospitali ya Rufani Amana jijini Dar es Salaam kudaiwa kutoroka.

Tukio hilo lilidaiwa kutokea usiku wa kuamkia jana hospitalini hapo na kuleta hofu kwa wananchi juu ya walikokwenda wagonjwa hao na watu waliokutana nao mitaani.

Mjema alithibitisha jana kuwapo kwa tukio la wagonjwa hospitalini hapo kulazimisha kuondoka ili kurejea nyumbani, lakini hakuthibitisha taarifa za wagonjwa kuondoka hospitalini.

"Ni wagonjwa ambao walikuwa pale (Hospitali ya Amana) ambao hawataki kuendelea kukaa hapo, walifika pale hawaumwi sana, walikuwa wanataka waruhusiwe.

"Sasa, kumbuka kwamba, ukiwa umefika pale halafu una corona, lazima ukae kidogo hospitalini uangaliwe, wakuone kama upo vizuri ndipo wakuruhusu.

"Hawa hawataki kubaki hospitali, wanataka waruhusiwe kuondoka, sina uhakika kama ni vurugu imetokea ila kilichotokea ni walikuwa wanapiga kelele, wanataka kuondoka, warudi nyumbani. "Tunachojua wagonjwa walikuwa wanasema wanataka kurudi nyumbani kwa kutishia wataondoka, ngoja tuone kwa walinzi wanaolinda hapo kama kuna watu wametoroka na kama wapo ni wangapi na wamekwenda wapi?" alisema.

Mjema alisema hata kama wametoka hospitalini hapo, wanajulikana wanatoka wapi, hivyo kikubwa ni kuwafuatilia.

"Kama kuna mtu alishukiwa kuwa na corona mtaa 'A', ikionekana hayupo hospitali, atatafutwa mtaa 'A', kwa sasa hali ni shwari hapa hospitali lakini tunazidi kuwaambia wafuate utaratibu wa hospitali ulivyo. Aliwataka Watanzania watulie na waisikilize serikali inasema nini kwa sababu mgonjwa anapofika Amana, ataangaliwa na akionekana yupo salama, ataruhusiwa kwenda nyumbani. "Kuwa na vurugu sioni kama inasaidia, fikiria mtu ana viashiria vya ugonjwa halafu akimbilie mtaani, hata huko mtaani watamkimbia watasema hatukutaki, rudi hospitali utibiwe.



**POLISI WACHUNGUZA**

Kaimu Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Camilius Wambura, aliiambia Nipashe jana kuwa, Jeshi la Polisi linafuatilia taarifa za wagonjwa kutoroka katika Hospitali ya Amana.

"Tumepokea taarifa za watu kukimbia Amana, tunafanya uchunguzi kufuatilia kama taarifa hizo ni za kweli, ila kama unataka kujua wametoroka wangapi, wagonjwa waliokuwa wamelazwa walikuwa wangapi, wanaoweza kutoa takwimu sahihi ni mamlaka husika," alisema.

Katika hatua nyingine, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, amewaonya watoa huduma za afya wanaowakimbia wagonjwa wanaowahisi kuwa na virusi vya corona, akibainisha kuwa mwongozo wa utoaji huduma za afya unakataza watoa huduma kuwakimbia wagonjwa. Ummy aliyasema hayo jijini Dar es Salaam jana, alipopokea vifaa vya kunawia mikono kutoka kwa shirika lisilo la kiserikali la Water Mission Tanzania.

■**Imeandikwa na Romana Mallya na Elizabeth Zaya**

# Majaji rufani ya kina Mbowe wapangwa

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Dar es Salaam, imepanga kusikiliza rufani ya vigogo wanane wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), akiwamo Mwenyekiti wa chama hicho, Freeman Mbowe, dhidi ya Jamhuri Mei 13 mwaka huu.

Rufani hiyo imepangwa kutajwa mbele ya Jaji Mfawidhi Lameck Mlacha Aprili 28, mwaka huu na kisha itasikilizwa mbele ya Jaji Ilvin Mgeta wa mahakama hiyo.

Mbowe na wenzake wamekata rufani Mahakama Kuu kupinga hukumu ya kulipa faini ya jumla ya Sh. milioni 320 au kwenda jela miaka mitano kwa kila kosa walilokutwa na hatia.

Rufani hiyo iliyosajiliwa kwa namba 76 mwaka huu na iliwasilishwa na Wakili wa Walalamikaji, Peter Kibatala ikiwa na sababu 14.

Kwa mujibu wa hati ya rufani, walalamikaji wanadai Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam, ilikosea kuwatia hatiani Mbowe na wenzake kwa sababu haikuchambua ushahidi wa Jamhuri wakati wa kuandika hukumu hiyo.

Katika rufani hiyo, hoja nyingine ni Mahakama ya Kisutu katika hukumu yake kutoonyesha sababu zilizopelekea washtakiwa kutiwa hatiani.

"Upande wa Jamhuri ni jukumu lao kuthibitisha makosa bila kuacha shaka na kwamba si kazi ya mshtakiwa kujitetea," ilielezwa katika sehemu ya hoja za walalamikaji. Katika hoja yao nyingine, wanadai Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba, hakutilia manani utetezi wa washtakiwa, akiwamo Esther Matiko na John Mnyika, katika ushahidi wa Jamhuri hakuna ulipoelezwa kama washtakiwa walikuwapo kwenye tukio.

Pia, wanadai mahakama ilikosea kuwatia hatiani washtakiwa katika shitaka lililokuwa na mashtaka manne ndani yake ikiwamo, kufanya maandamano, kusababisha kifo cha Akwilina, kusababisha askari polisi wawili kujeruhiwa.

Hoja nyingine ni kwamba mahakama ilipokea CD iliyoonyesha maandamano ya washtakiwa kinyume cha sheria na kwamba utaratibu wa kisheria haukufuatwa na kielelezo hicho kilipokewa kiholela.

Mbali na Mbowe, Matiko na Mnyika, washtakiwa wengine ni, Mchungaji Peter Msigwa, Halima Mdee, John Heche, Naibu Katibu Mkuu wa Chadema Zanzibar, Salum Mwalimu, na Mbunge wa Bunda, Esther Bulaya.

Katika kesi ha msingi, Mbowe na viongozi wenzake walishitakiwa kwa mashitaka 12 ya uchochezi na moja la kula njama.

Upande wa Jamhuri ukiongozwa na Wakili wa Serikali Mkuu, Faraja Nchimbi, ulifunga ushahidi wakiwa na jumla ya mashahidi wanane.

Upande wa utetezi uliongozwa na Wakili Kibatala na uliita mashahidi watano.

Hati ya mashtaka ya awali ilikuwa na mashtaka 12 yakiwamo ya kufanya mkusanyiko usio halali, lakini hati mpya ilikuwa na mashtaka 13 likiwamo shtaka la kufanya maandamano yasiyo halali wakiwa na lengo la kuvamia Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni.


Enabel

**Vacancy – Position no: 1708**

**Monitoring and Evaluation Technician in Kigoma Region**

***Enabel – Belgian Development Agency – recruits a Tanzanian national***

- Duty station: Kigoma town/district
- Contract term: 1 year – extendable – competitive salary package.
- Profile: Bachelor degree Information Technology, Agricultural economics, Records Management, Informatics, Computer Science or equivalent.
- Minimum experience: 1-year in data management
- Job content: mobile data Collection, People Management in Agricultural extension, Training, Data Analysis & visualisation, Reporting and Mapping.
- Competencies: Advanced user of Excel and good knowledge of monitoring and evaluation concepts; Experience in conducting qualitative/quantitative analysis integrating a gender perspective and/or a human-rights based approach, vulnerable groups or similar is a plus; Knowledge of ODK and GIS is an asset; Good reporting skills in English/ Kiswahili.

Details vacancy at: **https://btctanzania.wordpress.com/**
Submit your applications **mentioning the position number to: recruitment.tza@enabel.be**
**Deadline: 3rd May 2020**
Only shortlisted candidates will be contacted.

Female applicants are especially encouraged to apply. Enabel has zero tolerance for any form of discrimination and does not discriminate on the basis of HIV/AIDS status.

215707502


# Serikali yatangaza bei elekezi sukari

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Kilimo, Japhet Hasunga, ametangaza bei elekezi ya sukari kwa kila mkoa nchini, huku akiwaonya watakaobainika kuuza kinyume cha utaratibu huo kuwa hatua za kisheria zitachukuliwa ikiwamo kunyang'anywa leseni ya biashara.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa jana, kutokana na kupandishwa kwa bei ya bidhaa hiyo kiholela, Hasunga alisema serikali imechukua hatua hiyo ili kudhibiti hali hiyo.

Alisema bei ya bidhaa hiyo imepanda kwa wastani wa Sh. 4,000 hadi 4,500 kwa kilo kwa bei ya rejareja.

"Sheria ya Sukari Na. 26 ya Mwaka 2001 chini ya kifungu cha 11A, inampa mamlaka waziri mwenye dhamana ya kilimo kutangaza bei ya ukomo wa juu ya sukari," alisema.

Hasunga alisema bei hiyo elekezi imepangwa kwa kuzingatia gharama zote za uagizaji wa sukari ya kuziba pengo zinazotumiwa na wazalishaji kuagiza sukari kutoka nje ya nchi na umbali wa kila eneo.

Waziri huyo alibainisha bei kwa kila mkoa kwenye mabano kuwa ni Dar es Salaam (Sh. 2,600), Iringa, Njombe, Mwanza, Simiyu, Shinyanga, Geita, Singida, Tabora na Dodoma (Sh. 2,900), Lindi na Mtwara (Sh. 2,800), Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Pwani, Tanga na Morogoro (Sh. 2,700).

Pia, mikoa ya Songwe, Mbeya, Mara, Kagera, (Sh. 3,000), Rukwa, Katavi, Ruvuma na Kigoma (Sh. 3,200).

Aliwataka wafanyabiashara wote nchini kuzingatia maelekezo hayo ya serikali na atakayekiuka atakuwa ametenda kosa na hivyo atafikishwa katika vyombo vya sharia. "Miongoni mwa adhabu atakazopata itahusisha ama kunyang'anywa leseni ya biashara, kulipa faini au adhabu zote kwa pamoja, wafanyabiashara wenye tabia za kupandisha bei kiholela waache mara moja," alionya.

Alisema serikali haipo tayari kuona wananchi wake wanaumia kwa manufaa ya watu wachache na kuiagiza Bodi ya Sukari kukaa na waagizaji ili kufikia bei elekezi kwa bei ya jumla kulingana na mkoa husika.

Vilevile, Waziri Hasunga alisema mahitaji ya sukari ya matumizi ya kawaida nchini yanakadiriwa kufikia tani 470,000 kwa mwaka, ikiwa ni wastani wa mahitaji ya tani 38,000 kwa kila mwezi na sukari kwa ajili ya dharura ni tani 14,000.

"Uwezo wa viwanda vya ndani kwa msimu wa 2019/20 kwa mujibu wa makadirio ya mwanzoni mwa msimu Julai 2019, ni kuzalisha takribani tani 378,000 za sukari, kiasi hiki ni sawa na asilimia 82.9 ya mahitaji halisi ya tani 456,000 ambayo hayajumuishi kiasi cha dharura cha tani 14,000," alisema.

Alibainisha kuwa uwezo huo wa uzalishaji wa viwanda vya ndani unaacha pengo la kiasi cha tani 78,000 ili kutosheleza mahitaji halisi ya tani 456,000 bila kiasi cha dharura cha tani 14,000.

"Uwezo huu wa uzalishaji wa viwanda vya ndani ulitarajiwa kufikiwa pale tu panapokuwa na hali nzuri ya hewa na ufanisi mzuri wa viwanda," alisema.



## DK. REGINALD ABRAHAM MENGI

*"Kila siku jitahidi kufanya vizuri zaidi kuliko ulivyofanya jana."*

# Hakika aliipenda tasnia ya habari

**Na Mwandishi Wetu**

AKIWA Mwenyekiti wa Chama cha Wamiliki wa Vyombo vya Habari Tanzania (MOAT), Dk. Reginald Mengi, mipango yake ilikuwa ni kuendeleza vyombo vya habari nchini kwa kushirikiana na Shirika la Habari la Kimataifa (IPI) kutoka Vienna, Austria.

Lengo kubwa lilikuwa ni kuona waandishi wa habari wanakua kitaaluma. Aliamini waandishi wanapaswa kuendelezwa kielimu na alifanyakazi kwa karibu na Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF).

Kabla ya kuteuliwa na Rais Julius Nyerere mwaka 1984 kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi nchini, kila aliyekuwa anasoma hesabu alikuwa anajitangaza kuwa ni Mhasibu.

TEF ilimuuliza Dk. Mengi kama alilolifanya kwa kuweka utaratibu wa Wahasibu kusomea CPA kuwa na viwango maalum vya elimu, ingefaa hata waandishi kuwa na viwango hivyo? Alilipenda wazo hilo na kuitaka TEF washirikiane na taasisi kama IPI kuona jinsi gani wanavyoweza kuanzisha elimu ya aina hiyo kwa waandishi.

Makamu Mwenyekiti wa TEF, Deodatus Balile, akimzunguzia Dk. Mengi, anasema hajaona mmiliki wa vyombo vya habari mwenye uwezo wa kiuchumi anayeliendeleza lengo hilo.

Anasema licha ya kuwa na kampuni zaidi ya 40 alizoziorodhesha kwenye Business Card yake, lakini hakika aliipenda tasnia ya habari. "Nawafahamu wamiliki wa vyombo vya habari wenye uwezo mkubwa mno kifedha, lakini sijaona wakiitisha vikao vya kuendeleza tasnia ya habari kama alivyokuwa akifanya Dk. Mengi."

"Naweza kusema kwa ujasiri, tasnia ya habari nchini imekosa mtetezi. Haina mtu wa kuisemea. Tumefika mahala sasa hata wale watangazaji kidogo waliosalia hawathamini tena vyombo vya habari maana wanajua havina mtetezi. Kilichotokea ni sawa na vile Mchungaji amepigwa na kondoo wametawanyika."

"Hili limenifanya nimkumbuke Mzee Mengi. Katika hali kama hii ambayo nafahamu inavikumba vyombo vya habari vingi nchini vilivyoyumba kiuchumi, angesimama akakemea. Angewaeleza wahusika faida tunayowapatia kupitia vyombo vya habari. Mfano mzuri ni katika hili janga la corona. Kwa sasa hakuna anayefanya mkutano wa hadhara, hakuna anayetembelea wapigakura, lakini wanategemea vyombo vya habari kufikisha ujumbe wa corona kwa wananchi na unafika kwa wakati mwafaka.



Dk Reginald Mengi akizungumza na wahariri wa vyombo vya Habari. **NA MPIGAPICHA WETU**

> Hili limenifanya nimkumbuke Mzee Mengi. Katika hali kama hii ambayo nafahamu inavikumba vyombo vya habari vingi nchini vilivyoyumba kiuchumi, angesimama akakemea.



Dk Reginald Mengi akizungumza na viongozi wa Baraza la Habari nchini katika moja ya matukio.

Ule moyo wa mshikamano ndani ya vyombo vya habari sijauona tena. Sasa hivi tasnia ya habari ina usukani mbili. Inanikumbusha wimbo wa mwanamuziki, Saida Karoli, aliyeimba "Dereva babili, dereva babili, dereva balili, dereva babili kubuga emotoka emo no rushengooooo." Akimaanisha, dereva wawili kuendesha gari moja ni hatari.

Anasema kwa sasa vyombo vya habari havina mwenyewe. Vina usukani mbili, vinaendeshwa na madereva wawili. Mzee Mengi aliyekuwa mlezi wa vyombo vya habari hakupata kuwa na malengo ya kisiasa, hili nalo katika kitabu chake "I can, I must, I will: The Spirit of Success" amelisemea, ingawa muda wote wapo waliodhani anayo malengo ya kisiasa. Ni ukweli kuwa kwa hapa nchini zaidi ya asilimia 98 ya wamiliki wanafahamika matamanio yao ya kisiasa.

Vyombo vya habari vingi sasa vimepoteza mkondo wa kusema ukweli bila kufikiria masilahi ya kisiasa mbele ya safari.

"Wamiliki wengi wa vyombo vya habari ni wagombea watarajiwa au ni wanasiasa tayari kupitia vyama mbalimbali vya siasa. Wanasiasa wa aina hii, ambao wengi wao ama ni wamiliki au walikuwa watumishi katika vyombo vya habari wakavitumia kuingia kwenye siasa. Kwa bahati mbaya wanadhani wote walioko kwenye vyombo vya habari wana malengo ya kisiasa kama wao, jambo linalotuumiza baadhi yetu."

Anamkumbuka Dk. Mengi kusimamia vyema eneo hilo la vyombo vya habari kubaki kusema ukweli bila kujali gharama ya ukweli huo. "Vyombo vyake vya ITV, East Africa Television, Radio One, Capital Television, magazeti ya Nipashe, The Guardian na vingine, hakika vilisema ukweli nyakati zote na kuwapa fursa wananchi kuona thamani ya chombo vya habari.

Anasema Dk. Mengi hakuishia kwenye vyombo vyake pekee, alipobaini kuwa kuna chombo iwe gazeti, radio au televisheni kinakengeuka au kinasema nusu ukweli, aliitisha mkutano si tu wa wamiliki wa vyombo vya habari, bali pia hata wahariri na wakati mwingine waandishi wa habari na kukumbushana dhamana na umuhimu wa vyombo vya habari kusimamia ukweli.

# Wakurugenzi h/shauri 33 kupelekwa kwa Magufuli

Na Augusta Njoji, DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, amesema atapeleka kwa Rais majina ya Wakurugenzi wa Halmashauri 33 ambao wamechangia chini ya asilimia 20 ya bajeti ya mikopo ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Aidha, amesema katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020, Halmashauri ya Jiji la Dodoma imeongoza kwa kukusanya pato ghafi kiasi cha Sh. bilioni 36.04 huku Jiji la Dar es Salaam likiwa la mwisho ambapo limekusanya Sh.Bilioni 8.83.

Akitoa jana taarifa ya mapato na matumizi kwa mwezi Julai 2019 hadi Machi 2020, Jafo alisema Wakurugenzi hao wameshindwa kutekeleza sheria iliyotungwa na Bunge kwa kuchanga chini ya asilimia 20 ya bajeti hiyo. "Mtakumbuka nilisema nitakaposoma taarifa yangu ya mwisho nitaainisha Halmashuari ambazo zimeshindwa kutekeleza sheria iliyotungwa na Bunge na majina yao nitapeleka kwa Rais kuangalia jinsi gani hawa Wakurugenzi wameshindwa kutimiza.

"Tangazo hili nitalitoa mapema mwezi Juni, mwaka huu, hawa watakuwa kwa makusudi wameshindwa kutekeleza sheria iliyotungwa na Bunge," alisisitiza.

Alieleza kwa kipindi hicho Halmashauri zilitoa Mikopo kiasi cha Sh. bilioni 27.40 kwa Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu ikiwa ni asilimia 44 ya Bajeti ambayo ni Sh. bilioni 62.40.

"Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo imeongoza kutoa mikopo kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa kuchangia asilimia 134 ya Bajeti, Aidha, Halmashauri 34 zimechangia asilimia 75 na zaidi ya Bajeti," alisema.

Alisema Halmashauri 51 zimechangia kati ya asilimia 50 hadi 74 na Halmashauri 67 zimechangia kati ya asilimia 20 hadi 49 ya Bajeti.

"Hata hivyo, zipo Halmashauri 33 ambazo zimechangia chini ya asilimia 20 ya Bajeti hiyo,"alisema.

Kuhusu makusanyo, Jafo alisema Halmashauri 58 zimekusanya mapato ya ndani kwa asilimia 75 au zaidi kwa kulinganishwa na makisio kwa mwaka wa fedha 2019/20.

Aidha, alisema Halmashauri 96 zimekusanya asilimia 50 au zaidi lakini chini ya asilimia 75 na Halmashauri 31 zimekusanya chini ya asilimia 50 ya makisio ya mwaka.

**NJOMBE YANG'ARA**

Alisema mkoa wa Njombe umekusanya wastani wa asilimia 87 ya makisio ya Halmashauri za Mkoa huo huku mkoa wa Simiyu ukiwa umekusanya wastani wa asilimia 51 kwa kigezo cha asilimia.

**DAR YAONGOZA**

Alisema kwa kigezo cha wingi wa mapato, Mkoa wa Dar es Salaam umekusanya kiasi cha Sh. bilioni 126.77 huku Mkoa wa mwisho ni Mkoa wa Rukwa ambao umekusanya Sh. bilioni 6.34.

**HALMASHAURI ZA MAJIJI**

Alisema katika kipindi hicho Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam imeongoza kwa kigezo cha asilimia imekusanya kwa asilimia 78 ya makisio yake ya mwaka. "Halmashauri ya Jiji la Dodoma imekuwa ya mwisho katika kundi hili ambapo imekusanya kwa asilimia 55 ya makisio yake ya mwaka,"alisema.

Aidha, alisema Halmashauri ya Jiji la Dodoma imeongoza kwa kukusanya pato ghafi kiasi cha Sh.Bilioni 36.04 huku Jiji la Dar es salaam likiwa la mwisho ambapo limekusanya Sh.Bilioni 8.83.

**HALMASHAURI ZA MANISPAA**

Alisema Halmashauri ya Manispaa ya Iringa imeongoza kundi hilo kwa kukusanya kwa asilimia 100 ya makisio yake huku Manispaa ya Lindi imekuwa ya mwisho ambapo imekusanya kwa asilimia 49 kwa kigezo cha asilimia.

Kwa upande pato ghafi, Jafo alisema wa Halmashauri za Manispaa ya Ilala imeongoza kwa kukusanya Sh.Bilioni 43.14 huku Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma Ujiji imekuwa ya mwisho katika kundi hili ambapo imekusanya Sh.Bilioni 1.20

**HALMASHAURI ZA MIJI**

Alisema Halmashauri ya Mji wa Njombe imeongoza kwa kukusanya kwa asilimia 130 huku Halmashauri ya Mji wa Handeni imekuwa ya mwisho kwa kukusanya asilimia 43.

Hata hivyo, alisema kwa pato ghafi, alisema Halmashauri ya Mji wa Geita imeongoza kwa wingi wa Mapato kwa kukusanya Sh.Bilioni 7.02 huku Halmashauri ya Mji wa Mbulu imekuwa ya mwisho katika kundi hilo ambapo imekusanya Sh. Milioni 671.78.

**HALMASHAURI ZA WILAYA**

Aidha, alisema, Halmashauri ya Wilaya ya Masasi imeongoza kwa kukusanya asilimia 126 huku Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga imekuwa ya mwisho katika kundi hilo kwa kukusanya asilimia 30 ya makisio.

Pia kwa upande wa pato ghafi, alisema Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze imeongoza kwa kukusanya Sh. bilioni 5.78 huku Gairo imekuwa ya mwisho kwa kukusanya Sh. milioni 343.70.

# Mitaa yapewa jukumu udhibiti watoto corona

Na Elizabeth Zaya

MKURUGENZI Mtendaji wa Taasisi ya Wanawake katika Jitihada za Maendeleo Tanzania (Wajiki), Janeth Mawinza, ameomba viongozi wa serikali za mitaa kuhakikisha wanawadhibiti watoto kuzurura mitaani katika kipindi hiki ambacho shule zimefungwa kwa ajili ya tishio la ugonjwa wa corona.

Alisema ni vema viongozi wa mitaa wakahusika na kudhibiti suala hilo kwa kuwa wao ndio wako karibu na mitaa wanakoishi wanafunzi hao.

"Kumekuwa na changamoto sasa kwa watoto kuzurula mitaani tangu serikali ilipofunga shule kutokana na tishio la ugonjwa wa corona, badala ya kuona kwamba wanatakiwa kutulia ndani na kujisomea, wao ndiyo wanaona ndiyo muda wa kuutumia kwenye michezo," alisema Mawinza.

Aliongeza: "Kwa hiyo ndiyo maana tunaomba kwamba viongozi wa serikali wafanye kazi hiyo ya kuwaambia wazazi na watoto kwa ujumla kwamba hatakiwi kuonekana mtaani mtoto yeyote, wakae majumbani wajisomee."

"Kufungwa kwa shule siyo kufungwa kwa akili, isipokuwa wa majengo tu ndiyo yamefungwa na kwamba huwezi kuwa karibu na mwalimu uso kwa uso, lakini bado kuna nafasi ya kujisomea kwa ajili ya maandalizi ya siku mbele za kuendeleza elimu yao."

Alisema ni vema wazazi wakawa msaada kwa watoto wao katika kuhakikisha wanawapangia muda wa kijisomea na kuwazuia wasitoke ndani ya nyumba zao.

"Tupunguze pia kelele katika mitaa yetu ili tuwasaidie watoto wasome vizuri na wasione kwamba hicho nacho ni kikwazo kwa sababu hatujui corona inaisha lini," alisema Mawinza.

**VACANCY**
**(For reputed Developer)**

**Project manager : Posts: 2**
**Qualification :** Civil or Mechanical Engineer, Electrical Engineer 7 years experience in project or site management and should have very high communication skills. Also reference should be from 3 reputed people in the construction industry

**Electrical engineer : Posts: 5**
**Qualification:** Graduation in Electrical
7 years experience

**Electrical technician : Post : 5**
**Qualification:** Diploma in Electrical
5 years Experience

**Plumber : Post :5**
**Qualification:**Diploma in Plumbing
10 years Experience

**AC Technician : Post :3**
**Qualification:** Highly qualified Diploma in Air condition technology
5 years Experience

Very fluent in English and Swahili for all above posts.

***Only Tanzanian citizens for all posts***

***Deadline: 7th May 2020***

**Resumes should be sent to Email : Safari@sura-tz.com & vasudha0606@yahoo.com**

**bgtl BEST GROUP (T) LIMITED**
Debts collectors, Auctioneer, Commission Agent & Legal Consultant

**NOTISI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

Kwa Idhini tuliyopewa na **MAENDELEO BANK PLC** Tunatoa notisi ya siku kumi na nne (14) kuanzia Tarehe ya Tangazo hili kwa wadaiwa tajwa hapo chini, walipe madeni yao wanayodaiwa. Kushindwa kulipa kwa muda huo tutalazimika kuuza dhamana (mali) zao kwa Mnada wa hadhara. Mnada utafanyika tarehe husika kuanzia saa 4:00 asubuhi na kuendelea.

| Na. | JINA LA MDAIWA/MDAMINI | MAELEZO YA DHAMANA MAHALI ILIPO |
|---|---|---|
| 1. | GREEN BIRD GIRLS SECONDARY SCHOOL/KAULA DEVELOPMENT TRUST FUND LIMITED | Nyumba ya makazi yenye Hati na.1600, kiwanja na.25, Kitalu D iliyopo eneo la Mwanga mjini Kilimanjaro. |
| 2. | ZUWENA HABIB MNDEME | Nyumba ya makazi yenye Hati na.124790,Kiwanja na.685, Kitalu A Iliyopo maeneo ya sinza Dar es salaam |
| 3. | DIANA FRANCIS MAHATANE | 1. Nyumba ya makazi yenye Hati na.49589,Kiwanja na.413, Kitalu A Iliyopo maeneo ya Ndurumanga Arumeru Arusha.<br>2. Kiwanja chenye Hati ya mauziano kilichopo mtaa wa Mwera Kata ya Somangila manispaa ya Kigamboni |

**MASHART YA MNADA**

1. Dhamana zitauzwa kama zilivyo.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo yaasilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14). Kukamilisha malipo yote. Kushindwa kufanya hiyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25%, na mnada kurudiwa, au mshindi wa pili atapewa ushindi.
4. Gharama za kuona, kukagua, kuhamishaumiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji na zingine zinazoambatana na hilo ni jukumu la mnunuzi.

**Kwa Taarifazaidiwasilianana:** **AU** **MkurugeziMtendaji**

**MkurugeziMtendajimaendeleo Bank plc,**
**Head Office,**
**Luther House Posta Sokoine drive,**
**P.O. BOX 216,**
**DAR ES SALAAM**
**phone; +255 222110518**
**Email: info@maendeleobank.co.tz**

**Best Group (T) LTD**
**Alli Hassan Mwinyi Road.**
**Green Acres Buliding, 2nd Floor.**
**P.O. BOX 1088**
**DAR ES SALAAM**
**MOBILE + 255 715-363537/ +255 765-363537**

## TANGAZO


POPOTE
INATIKI
Kimbiza miamala yako upendavyo.
SimBanking
ATM
POS
INTERNET BANKING
WAKALA
SCAN, LIPA, SEPA
*150*03#
PAKUA KWENYE
CRDB BANK
Tunakusikiliza

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Msako wanaouza sukari bei juu wakati mwafaka

**WAZIRI** Mkuu Kassim Majaliwa, amewaagiza wakuu wa mikoa kuchukulia hatua dhidi ya wafanyabiashara waliopandisha bei ya sukari na kufikia Sh. 4,500 kwa kilo.

Amesema haoni sababu ya kupanda kwa bei kwa kuwa bidhaa hiyo ipo ya kutosha nchini.

Hatua ya Majaliwa imetangazwa ikiwa ni wiki tangu sukari kupandishwa bei maeneo mbalimbali nchini.

Hata hivyo, serikali kupitia mamlaka zake kama Wizara ya Viwanda na Biashara na Bodi ya Sukari zimekuwa zikisisitiza kuwa nchi ina sukari ya kutosha, hivyo kushangaa sababu za baadhi ya wafanyabiashara wa bidhaa hiyo kupandisha bei kiholela.

Akizungumza juzi na viongozi wa dini kwenye maombi maalum kwa kitaifa dhidi ya virusi vya corona jijini Dar es Salaam, Majaliwa aliwataka wafanyabiashara kutopandisha bei ya sukari na bidhaa nyingine. Alisema sukari ipo, tena ya kutosha na iliyokuwa imepungua imeshaagizwa na imeingia nchini, na kwamba bei inaendelea kuwa ileile, viwanda vya ndani vikianza kuzalisha, bei itaendelea kuwa ileile.

Alisema ameona kwenye mitandao kilo imefikia Sh.4,500, hivyo kuwaagiza wakuu wa mikoa kuwachukulia hatua wafanyabiashara hao. Aliwataka wafanyabiashara kote nchini wahakikishe vyakula muhimu kwenye kipindi cha Ramadhani vinauzwa kwa bei inayotambulika bila kupandishwa.

Aliwataka wakuu wa mikoa na wakuu wa wilaya kufanya ziara za mara kwa mara kwenye masoko yaliyopo kwenye maeneo yao.

Alionya kuwa, hakuna sababu ya kupandisha huduma kwenye masoko eti kwa sababu baadhi ya Watanzania wanaingia mwezi Mtukufu.

Sababu za kupanda kasi kwa bei ya sukari hazijafahamika kwa kuwa hakuna taarifa rasmi kutoka kwa mamlaka husika kuwa nchi kwa sasa ina uhaba wa sukari.

Kwa uzoefu wetu, bei ya sukari imekuwa ikipanda katika kipindi ambacho viwanda vyetu vinapofungwa kwa ajili ya ukarabati kusubiria msimu mpya.

Hata hivyo, kwa kipindi hicho unapojitokeza uhaba, serikali huingilia kati na kuruhusu uagizaji wa bidhaa hiyo kutoka nje.

Kwa hali inayooendelea sasa, tunapata hisia kuwa kuna baadhi ya wafanyabiashara ya sukari wanaificha ili kuonyesha kuwa kuna uhaba, hivyo watumia mwanya huo kuiuza kwa bei kubwa.

Lakini pia tunahisi kuwa wafanyabiashara wasio na nia njema kwa Watanzania wenzao na taifa kwa ujumla, wanaona kuwa kipindi hiki kuelekea mfungo wa Ramadhani, kutakuwa na mahitaji makubwa ya sukari, hivyo kuvuna faida kubwa kama wataiuza kwa bei ya juu. Kwa kuwa hakuna sababu ya msingi inayothibitisha kuwa nchi ina uhaba wa sukari, msako aliouagiza Waziri Mkuu ni hatua nzuri na yenye tija.


Bila shaka walengwa wa msako huo wanajulikana kwa kuwa serikali ina mkono mrefu wa kupata taarifa. Isitoshe, imeshafanya misako hiyo mara kadhaa kwenye maghala husika hususan jijini Dar es Salaam na kuwatia mbaroni waficha sukari.

Kadhalika, hatua ya jana ya Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, kutangaza bei elekezi ya bidhaa hiyo kwa kila mkoa, tunaamini kabisa kwamba itakuwa kibano tosha dhidi ya wanaofanya mchezo huo.

Ni matarajio yetu kuwa hatua hizi zitawabana wanaoleta mzaha kwenye suala la sukari, hivyo kutowapa usumbufu watumiaji wa bidhaa hiyo nchini pamoja na waumini wa Kiislamu ambao wanauanza mfungo wa Ramadhani wakati wowote kuanzia sasa.

Wale watakaoendelea kuwa wakaidi katika hili, serikali isisite kuchukua hatua kali dhidi yao ili liwe fundisho kwao. Hakuna sababu kila mwaka wananchi kusababishiwa usumbufu huu na watu wachache kwa manufaa yao, wakati serikali inazo sheria za kuwaadabisha.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com





## Muungwana Lazima Nilonge

# Latra ingilieni kati Dar, nauli Sh.1000 sasa 'halali'

Na Sabato Kasika

**MWANZONI** mwa mwezi huu, Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (Latra), iliwataka watu binafsi kuomba leseni za muda mfupi kwa ajili ya kutoa huduma usafiri katika maeneo mbalimbali ya jiji la Dar es Salaam.

Sababu za kuchukuliwa hatua hizo, ni kutokana na uhitaji wa usafiri huo wa umma baada ya utekelezaji wa tahadhari dhidi ya maambukizi ya virusi vya corona, ambapo sasa daladala zimabeba abiria kulingana na idadi ya viti.

Hatua hiyo ya kukabiliana na virusi vya corona, imesababisha abiria kukosa usafiri na hivyo Latra ikalazimika kukaribisha maombi kwa wenye magari ya abiria wanaotaka kutoa huduma hiyo kwa muda.

Lakini, pamoja na nia nzuri ya taasisi hiyo ya kutaka abiria wasiendelee kuteseka vituoni, baadhi ya madereva wamegeuza ombi hilo la Latra kuwa fursa ya kutoza nauli kubwa, kuliko kiwango kinachotakiwa.

Madereva na makondakta wa magari wanaofanya hivyo, wale waliopewa kibali cha kuingia katikati ya jiji au wanaosafirisha kinyemela, kwa kigezo kwamba 'Latra imeruhusu.'

Tangu Latra kutangaza wenye magari ya abiria kuomba vibali vya muda, walioanza kutoa huduma hiyo wamepandisha bei. Wapo wanaotoza kutoka Sh. 600 hadi 1,000 kutoka Mbezi Mwisho kuelekea katikati ya jiji. Hiyo ni sehemu moja, maana kuna nyingine kati ya Ubungo Mataa na Gongolamboto, pia Makumbusho hadi Mbagala.

Wakati wakifanya hivyo, Latra inakemea kuwa ni 'uhuni' na kwamba nauli halali ya kuelekea au kutoka katikati ya jiji, bado ni Sh. 600. Hivyo, waliopindisha nauli watachukuliwa hatua za kisheria.

Mkurugenzi wa Udhibiti wa Usafiri wa Barabara, Johansen Kahatano, anaahidi kufuatilia kujua ukweli wao, kuhusu tozo za nauli, kinyume na iliyopangwa na serikali.

Ingawa Latra imechelewa kufuatilia jambo hili, lakini ninaamini kwa kiasi fulani itasaidia kuwaondolea machungu abiria ambao wamekuwa wakiteseka kwa nauli kubwa wanayotozwa kila siku bila hata huruma.

Kinachofanyika sasa ni kama abiria wamegeuzwa kuwa mtaji wa madereva na makondakta kwa kujipatia faida kinyume ambayo inatokana na kusafirisha abiria kwa nauli isiyo halali.

Huu ni uonevu kumtoza mtu nauli kubwa tofauti na ile iliyoelekezwa na mamlaka husika, hivyo ni vyema abiria nao kuwa na msimamo wa pamoja wa kutokukubali kutozwa nauli kubwa.

Abiria kukubali kulipa nauli ya Sh.1,000 badala ya 600 ni sawa na kuwapa jeuri madereva na makondakta wanaoendekeza tamaa ya fedha au kufanya biashara, kinyume na taratibu iliyopo.

Hebu fikiria abiria awe anaanzia safari Mbezi Mwisho au njiani, nauli hiyo hiyo ya Sh.1,000, wakati daladala nyingine zenye njia zinatoza kati ya Sh.400 hadi Sh. 600 kutegemea abiria safari yake inakoishia.

Kwa sasa magari hayo yameomba vibali vya muda kusafirisha abiria yana vitu gani vya ziada kuliko mengine, hadi yatoze kiasi hicho cha nauli? au yanapita barabara gani zaidi ya hizo zilizopo?

Latra ifanye haraka kukabiliana na changamoto hii, ambayo ni kero na inahabiriwa watu bajeti zao bila kutarajia na kwamba ni jambo halali na kumbe ni tamaa ya watu wachache ya kutaka kujinufaisha.

Kimsingi, utozaji nauli holela unaumiza abiria ingawa wapo baadhi yao huwalaumu wale ambao hawana kiasi hicho cha nauli kilichotangazwa na kondakta, eti washuke katika gani.

Hali hiyo inasababisha wenye magari waamue tu ili waende safari zao, lakini ukweli ni kwamba watu wanaumia.

Hivyo, si vyema kutumia kipindi hiki cha janga la corona, kujinufaisha badala yake watoze nauli halali.

Kwa kuwa Latra imeahidi kuvalia njuga suala hilo la kupandisha nauli kiholela, basi ni matumaini yangu ndani yangu muda mfupi, abiria wataondokana na adha hiyo inayowavurugia bajeti zao.

Kama ambavyo Latra inasema, magari hayo yaliomba vibali vya muda kwa ajili ya kusafirisha abiria jijini Dar es Salaam, sasa kutoza nauli kubwa ni uhuni ambao haupaswi kufumbiwa macho.

TANGAZO

LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE

Justice Lugakingira House, Kijitonyama, P. O. Box 75254, Dar Es Salaam, TANZANIA
Telephone: 2773048, 2773038, Fax: 2773037, E-mail: lhrc@humanrights.or.tz
Website www.humanrights.or.tz

**Rais John Pombe Magufuli**
**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**
**1 Barack Obama Drive**
**11400, Kivukoni, Dar es Salaam, Tanzania**

# YAH: MABORESHO YA MFUMO WA HAKI JINAI

**Mheshimiwa Rais,**
Kwanza nianze kwa kukupa pole kwa majukumu mazito uliyonayo ya kuhakikisha Tanzania inapata maendeleo endelevu na inakuwa na utawala bora. Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kimeandika barua hii ya wazi ili kufikisha ujumbe moja kwa moja usioghoshiwa. Barua hii ina lengo la kukubaliana na kauli uliyoitoa wakati wa maadhimisho ya siku ya sheria nchini (Februari 6,2020) kuhusu mlundikano mahabusu na upelelezi usiokwisha.

**Nitaanza na nukuu**
***"…kwa kweli bado kuna changamoto kubwa ya upelelezi wa kesi, jambo linalopelekea watu kunyimwa haki…ninawaomba Kitengo cha Upelelezi na wasimamizi wa sheria kitengo cha Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wahusika wote hili mlifanyie kazi. Watu wanateseka. Nimeshuhudia ukienda kwenye magereza, watu wanalia na wengine ni kesi za kusingiziwa"***—Mhe. John Pombe Magufuli, Februari 6,2020.

**Mheshimiwa Rais,**
Chimbuko la matatizo na changamoto tulizozibaini katika utendaji kazi wetu zinatokana na changamoto za kisheria, changamoto za watendaji na kiutendaji na uelewa mdogo wa sheria katika jamii. Changamoto hizi zimeongeza ugumu wa upatikanaji wa haki katika nchi yetu hususani haki jinai. Mfumo wa haki jinai unakabiliwa na changamoto nyingi kuanzia pale mtuhumiwa anapokamatwa, utaratibu wa kumshikilia, upelelezi, mwenendo wa kesi yake, haki ya kupata dhamana, anapokuwa mahabusu mpaka anapotiwa hatiani na baadae kutumikia kifungo chake.

Kimsingi, mchakato wa upatikanaji haki kupitia mfumo wetu wa sasa wa haki jinai unapingana na dhana iliyopo chini ya ibara ya 13(6) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 inayoweka dhana ya msingi ya kutokuwa na hatia mpaka itakapothibitishwa na mahakama. Ni wazi kwamba, dhana hii inalinda haki ya mtu yeyote kutotendewa kama mwenye kosa la jinai kama mahakama haijathibitisha kosa hilo kupitia utaratibu maalamu, inaweka msingi wa mtu kuwa huru na adhabu yoyote ikiwa mahakama haijathibitisha hilo na mwisho inalinda hadhi ya mtu ya kutoweza kufanyiwa makusudi ya kuwa na kosa kama haijathibitishwa na mahakama.

**Mheshimiwa Rais,**
Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kinatambua nia yako nzuri na mchango wako katika kusukuma maboresho ya mfumo wa haki jinai nchini, utayari wako umeonekana mara kwa mara ambapo unasisitiza viongozi kuwahakikishia watanzania wanapata haki zao mapema bila kero au ugumu wowote. LHRV tunaungana nawe kwa dhati kupitia kauli yako uliyoitoa katika maadhimisho ya siku ya sheria-Februari 6, 2020 kama ilivyonukuliwa hapo juu.

**Upelelezi kuchukua muda mrefu**

Suala la kesi kuchukua muda mrefu ni miongoni mwa sababu kubwa inayofanya idadi ya mahabusu kuwa wengi kuliko wafungwa. Kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa katika maadhimisho ya siku ya sheria zaidi ya asilimia 56 ya watu wote walio magerezani ni mahabusu. Hii inapingana na dhana ya kutokuwa na hatia na ya uhuru kama tulivyoeleza awali. Tunapendekeza maboresho ya sheria katika suala la upelelezi kuwekewa ukomo na mtu kuachiwa huru kwa kufutiwa kesi baada ya ukomo wa muda huo kupita. Pia, kabla ya mtu kushitakiwa upande wa upelelezi ni lazima kuonesha ushahidi wa awali kwa ajili ya kufungua kesi ya msingi yaani upelelzi kufanyika kabla ya kumfikisha mtuhumiwa mahakamani.

Kwa hali iliyopo sasa, mtuhumiwa anakaa mahabusu kwa muda mrefu akiwa anasubiri upelelezi ukamilike ili kesi yake ianze kusikilizwa. Kuna mifano mingi ya kesi zilizoko mahakamni kudhibitisha hili. Lakini kwa vile sheria inakataza kuzungumzia kesi zilizoko mahakamani na pia kukwepa kugonganisha mihimili miwili tunasita kuzitaja lakini mifano iko wazi.
Mheshimiwa Rais, jambo hili linahitaji maboresho ya kisheria na kiutendaji ili kutatua changamoto hii inayoathiri haki za watu katika mfumo wa haki jinai. Sheria inampa mamlaka Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP) kusimamia na kuratibu upelelzi wa makosa ya jinai lakini tumeona mara nyingi lawama zinatupwa kwa vyombo vya upelelezi.

**Ukamataji na kushikilia mtuhumiwa kwa muda mrefu**
Utaratibu uliyopo sasa unaruhusu polisi au chombo chochote husika kumkamata mtu na kumweka chini ya ulinzi baada ya kupokea taarifa ya uvunjifu wa sheria, au mashaka yoyote dhidi ya mtu huyo. Utaratibu huu unatoa mamlaka kwa jeshi la polisi kumshikilia mtuhumiwa kwa masaa 24 kabla ya kufikisha mahakamani vinginevyo polisi wamapaswa kutoa dhamana wakati upelelezi unaendelea. Mchakato huu umeathiriwa na tabia ya baadhi ya maafisa wa polisi kutumia kifungu hiki vibaya wakimshikilia mtuhumiwa bila dhamana kwa muda wa zaidi ya unaokubalika kisheria.

Hii imeainishwa katika kifungu cha 14(3) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, 1985, ni wazi kwamba kifungu hiki ni miongoni mwa sababu ya watuhumiwa kurundikana vituoni wakiwa wameshikiliwa na jeshi la polisi wakisubiri hatima ya kesi zao kabla ya kupelekwa mahakamani. Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kinapendekeza marekebisho ya kifungu hiki ili kutoa haki kwa watuhumiwa kufikishwa mahakamani mapema ndani ya saa 24.

**Makosa yasiyo na dhamana**
Kwa upande mwingine, makosa yasiyo na dhamana yamekuwa changamoto katika mchakato wa mtuhumiwa kupata haki. Ni muhimu kukumbuka kwamba, sheria ya mwenendo wa makosa ya jinai inaainisha makosa ya jinai yasiyokuwa na dhamana.

Kwa bahati mbaya, kuna makosa mengi ambayo hayana dhamana ukilinganisha na mifumo iliyopo katika nchi nyingine. Hii inamfanya mtu yoyote atakayetuhumiwa na kosa lolote lisilo na dhamana kutoweza kuwa huru hadi mwisho wa kesi yake. Tunafahamu kuwa, kesi za jinai huchukua muda mrefu ili kukamilika kwake hivyo, kukosa dhamana kunamfanya mtu kukaa mahabusu muda mrefu akisubiri kukamilika kwa kesi yake.

Hii inaathari katika maisha binafsi ya mtu, jamii na taifa kwa ujumla, kwani mtu hulazimika kuacha shughuli zake zote za ujenzi wa Taifa kwa kukaa mahabusu akisubiri kesi yake isiyo na

dhamana kukamilika. Tunafahamu familia mbalimbali zimeathirika kwa utaratibu huu na kubadilisha kabisa maisha ya familia hizo. Hivyo, kumfanya mtu kutumikia adhabu bila ya kuthibitika kuwa na kosa lolote la jinai. Mheshimwa Rais jambo hili linahitaji jitihada zako ili kunusuru maisha ya mtuhumiwa wa kosa lisilo na dhamana pamoja na jamii kwa ujumla.

Mwisho, tunaendelea kukupongeza kwa jitihada mbalimbali zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano unayoiongoza katika kuimairisha misingi ya uwajibikaji, uwazi na usimamizi wa haki. Tunatoa wito kwako kuendelea kusisitiza na kutoa kauli zinazosisitiza utii wa sheria kwa viongozi na wananchi wa Tanzania. Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kinaahidi kuendelea kuwa mstari wa mbele katika kuhamasisha wananchi na viongozi kuzingatia utii wa sheria, usawa wa kijinsia, uwajibikaji, haki za binadamu na utawala bora ili kufikia Tanzania ya viwanda kama ilivyoinishwa katika vipaumbele vya Serikali.

**Wako katika ujenzi wa Taifa.**

**Anna Henga**

**Mkurugenzi Mtendaji**
**Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu**



Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Dar es Salaam, Kate Kamba (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari jijini jana, kuhusu Chama hicho kutoa msaada wa barakoa milioni moja kwa wakazi wa jiji hilo wiki ijayo, ili kupambana na ugonjwa wa Covid -19. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Ajira mpya 4,400 kwa Polisi, Magereza, Uhamiaji, Zimamoto

**Na Salome Kitomari, DODOMA**

WIZARA ya Mambo ya Ndani ya Nchi, imetangaza ajira zaidi ya 4,400 kwa vyombo vya ulinzi na usalama nchini.

Akiwasilisha makadirio ya bajeti ya mwaka 2020/21, Waziri wa wizara hiyo, George Simbachawene, alisema ajira hizo zitakwenda pamoja na mafunzo mbalimbali kwa askari na watumishi mbalimbali.

Alisema kwa mwaka huo, Jeshi la Polisi linatarajia kuajiri askari 2,725, askari Magereza 685, Uhamiaji 495 na Zimamoto 501.

Simbachawene alisema katika mwaka 2020/21 Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na wadau wa ndani na nje ya nchi limepanga kuendelea kutoa mafunzo mbalimbali kwa maofisa, wakaguzi na askari 9,465 pamoja na watumishi raia 25.

Alisema kati ya hao 9,051 watapata mafunzo ndani ya nchi kupitia vyuo vya polisi na 414 nje ya nchi kwa udhamini wa taasisi na nchi mbalimbali.

Aidha, alisema katika kuimarisha utendaji kazi wa watumishi wa Jeshi la Polisi jumla ya maofisa, wakaguzi, askari na watumishi raia 5,470 wamepata mafunzo mbalimbali, kati ya hao 5,461 walipata mafunzo ndani ya nchi na tisa nje ya nchi.

**MAGEREZA**

Kwa upande wa Jeshi la Magereza, alisema katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020 jumla ya maofisa na askari 1,537 walipata mafunzo ya uongozi wa kijeshi katika vyuo vya Magereza na watumishi 951 walihitimu mafunzo ya taaluma mbalimbali katika vyuo vya ndani na nje ya Jeshi.

"Jeshi linatarajia kuajiri askari 685 wenye fani mbalimbali watakaopatiwa mafunzo ya awali katika Chuo cha Magereza Kiwira (Mbeya), mafunzo ya uendeshaji wa Magereza na Taaluma ya Urekebishaji kwa maofisa na askari 3,270 katika ngazi mbalimbali za uongozi," alisema.

Waziri Simbachawene alisema kuhusu hali ya ulinzi na usalama magerezani, hadi kufikia mwezi Machi, 2020 kulikuwa na jumla ya wafungwa na mahabusi 32,438 katika magereza yote nchini na kwamba kati ya hao, wafungwa ni 14,464 na mahabusi 17,974 ambapo ni asilimia 9 zaidi ya uwezo uliopo wa kuhifadhi wafungwa na mahabusu 29,902.

**UHAMIAJI**

Simbachawene alisema mwaka 2020/21 Idara ya Uhamiaji inatarajia kuajiri askari 495 na kuwapa mafunzo ya awali, ikiwamo kuendelea kutoa mafunzo mbalimbali kwa maofisa, askari na watumishi raia ili kuwaongezea ujuzi wa utendaji kazi kwa ufanisi zaidi.

**ZIMAMOTO**

Alisema katika kukabiliana na changamoto ya upungufu wa rasilimaliwatu, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linatarajia kuwapandisha vyeo maofisa na askari 1,311 na kuajiri askari wapya.

**VITAMBULISHO UTAIFA**

Alisema kwa mwaka 2020/21, Wizara kupitia Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (Nida) itaendelea na usajili na utambuzi katika wilaya na mikoa yote hapa nchini, ambapo jumla ya watu 6,076,666 wanatarajiwa kusajiliwa.

"Lengo ni kufikia idadi ya wananchi 27,796,983 watakaofikia umri wa miaka 18 mwezi Juni, 2021 kulingana na takwimu za ongezeko la ukuaji wa watu zilizotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS)," alifafanua.

Alisema idadi hiyo inafanya wananchi waliosajiliwa tangu kuanza kwa zoezi hilo kufikia 21,823,026 kati ya watu 25,237,954 waliolengwa kusajiliwa ifikapo mwezi Juni, 2020.

Alisema katika kipindi cha Julai, 2019 hadi

Machi, 2020, Nida imefanikiwa kusajili jumla ya wananchi 2,478,448, na kwamba idadi hiyo inafanya wananchi waliosajiliwa tangu kuanza kwa zoezi hilo kufikia 21,823,026 kati ya watu 25,237,954 waliolengwa kusajiliwa ifikapo mwezi Juni, 2020.

"Katika kipindi hicho,

Nida imesajili wageni wakazi 26,794. Pia, Mamlaka imetoa Namba za Utambulisho wa Taifa 17,871,770 na imechapisha pamoja na kugawa kwa wananchi Vitambulisho vya Taifa 6,103,225," alifafanua.

**USAJILI LAINI**

"Kwa kutumia mfumo wa usajili na utambuzi, Kampuni za Simu nchini zimefanikiwa kusajili laini zaidi ya 37,297,930 kwa kutumia alama za vidole,"alisema.

Alisema usajili wa laini umechangia kuongezeka kwa mapato yanayokusanywa na Nida kutoka lengo la Sh.milioni 500 mwaka 2019/20 hadi kufikia makusanyo halisi ya Sh. milioni 1.4 mwezi Machi, 2020.

# M.M.I Steel yakabidhi matangi 25 ya maji Pwani

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Evarist Ndikilo, ameonya baadhi ya abiria wanaokaidi agizo la kuvaa barakoa kama ilivyoshauriwa na wataalamu wa afya.

Akiongea wakati akipokea msaada wa matangi ya maji 25 kutoka katika Kampuni ya M.M.I Steel inayomilikiwa na Subhash Patel, ameagiza wahusika katika mkoa huo kufuatilia suala hilo kwa kuwa kuwaacha baadhi ya watu wakisafiri bila kuvaa barakoa ni kuendelea kuhatarisha afya za wengine na kusambaza virusi vya corona.

"Wananchi tuvae barakoa na kuzingatia asiwapo abiria anayesimama kwenye vyombo vya usafiri, hii ni kwa afya zetu hata mkisimama hamumkomoi mtu mwingine ni wewe na familia yako," alisema Ndikilo.

Pia, alisema hatarajii kuona mtoto akizurura mtaani kwa hali ilivyo sasa.

"Wazazi wazingatie kuwasisitiza watoto wao wasionekane mitaani, wasisubiri kila kitu kufuatiliwa na serikali," alisema.

Pia alisema bado misaada inahitajika katika mkoa huo ikiwamo vitakasamikono, barakoa na mafuta ya magari.

"Wawekezaji katika mkoa wetu na wadau mbalimbali, bado tunahitaji misaada yenu katika haya mapambano ya kujikinga na corona," alisema.

Alisema, matangi hayo yatagawanywa katika Ofisi ya Mkuu huyo wa Mkoa, Halmashauri za Wilaya, Hospitali ya Rufani ya Tumbi, Hospitali ya Utete, Mkuranga, Kituo cha Afya mkoani, Mlandizi na Kibiti, pamoja na Soko la Loliondo, Shirika la Nyumbu na Chama Matibabu Covid - 19 Lulanzi.

Ofisa Uhusiano wa Kampuni ya M.M.I Steel Abubakar Mlawa, alisema msaada huo wa tangi una thamani ya Sh. 6,250,000 na tayari wameshatoa msaada katika maeneo mengine wa matangi 1,000.

# Wawili wafa, nyumba 50 zikizingirwa maji

**Na Woinde Shizza,** ARUMERU

WATU wawili wamefariki dunia, huku nyumba zaidi ya 50 zikiharibiwa vibaya na mvua inayoendelea kunyesha mfululizo katika mikoa ya Arusha na Kilimanjaro.

Mbali na vifo, mamia ya abiria waliokuwa wakisafiri kutoka mikoa ya Kanda ya Kaskazini kwenda jijini Dar es Salaam na Tanga, wamekwama kwa zaidi ya saa sita, baada ya mvua kukatisha mawasiliano ya barabara kuu ya Arusha-Moshi eneo la Malula, wilaya ya Arumeru mkoani Arusha.

Jana, Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, alithibitisha watu hao kupoteza maisha kutokana na athari za mvua hiyo.

"Ni kweli wananchi hao wawili wamefariki dunia leo (jana) na wote ni wakazi wa Halmashauri ya Meru mkoani Arusha. Terevaeli Nasari (65), mkazi wa Kitongoji cha Meto, Kijiji cha Mulala alipoteza maisha baada ya maporomoko ya udongo kushuka mlimani na kuvunja ukuta wa chumba alichokuwa amelala na kufariki dunia papo hapo. Tayari mwili wake umepatikana na kupelekwa katika Hospitali ya Mkoa wa Arusha, Mount Meru.

Kwa mujibu wa Muro, mtoto mwenye umri wa miaka mitatu katia Kijiji cha Valeska, Kitongoji cha Mwamko, pia amefariki dunia baada ya kusombwa na mafuriko.

Alisema katika harakati za kumwokoa watoto wawili, mzazi wake aliyetambuliwa kwa jina moja la Simon, alifanikiwa kumwokoa mtoto mmoja na mwingine kufariki dunia.

Mkuu huyo wa Wilaya alisema madhara mengine yaliyojitokeza ni pamoja na nyumba zaidi 50 kuharibiwa vibaya na nyingine kuanguka kutokana na maji kuwa mengi.

Wakati hayo yakijitokeza, pia mamia ya abiria kutoka mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro walikwama kuendelea na safari kuelekea mikoa ya Dar es Salaam, mikoa ya Kanda ya Kati na Kanda ya Ziwa kwa zaidi ya saa sita eneo la Malula, Wilaya ya Arumeru kutokana na mafuriko kusitisha mawasiliano ya barabara ya Arusha-Moshi.

Eneo hilo la Malula, liko jirani na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA), ambako mafuriko ya maji yalifunga barabara hiyo, baada ya kupita juu ya makalavati na kuziba barabara, huku yakiharibu mali, mazao na miundombinu ya barabara.

# Jela maisha kwa kubaka binamu yake wa miaka 8

**Na Daniel Limbe,** CHATO

MKAZI wa Kijiji cha Katoro wilayani Geita, Jackob Thomas (20), amehukumiwa kifungo cha maisha jela baada ya kupatikana na hatia ya kumbaka mtoto wa miaka minane ambaye ni binamu yake.

Kabla ya kufikishwa mahakamani huko Aprili 21 mwaka huu na kufunguliwa kesi hiyo namba 117 ya mwaka 2020, Thomas alikamatwa Aprili 4 mwaka huu.

Hukumu hiyo ilisomwa jana na Hakimu Mkazi wa Mahakama ya wilaya hiyo, Erick Kagimbo, baada ya kusikiliza maelezo ya pande zote mbili.

Akisoma hukumu hiyo, Hakimu Kagimbo alisema kutokana na ushahidi iliotolewa na Upande wa Jamhuri pamoja na maelezo ya kukiri kosa la mshtakiwa, mahakama hiyo imelazimika kutoa adhabu ya kifungo cha maisha jela ili iwe fundisho kwa wengine wenye nia ya kutenda ukatili kama huo.

Alisema uamuzi huo unatokana na mshtakiwa kukiuka kifungu cha 130(1) na (2)(e) pamoja na kifungu cha 131(3) cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu iliyofanyiwa marejeo mwaka 2002.

Awali, Mwendesha Mashitaka wa Serikali, Anosisye Erasto, akishirikiana na Mwendesha Mashitaka wa Polisi, Semen Nzigo, walidai mahakamani huko kuwa mshitakiwa alitenda kosa hilo siku chache baada ya kumtembelea mjomba wake katika Kijiji cha Nyarututu wilayani Chato mkoani Geita.

Ilidaiwa kuwa siku ya tukio, wazazi wa mtoto aliyebakwa, hawakuwapo nyumbani na kwamba walimwacha mgeni wao akiwa chumbani kwake amelala kabla ya kufanya ubakaji huo.

Ilidaiwa mahakamani hapo kuwa, akiwa chumbani, watoto watatu waliingia kumsalimia kisha akawapatia Sh. 100 ili wakanunue pipi na waliporejea aliwaamuru watoto wengine wawili kwenda sebuleni huku akibaki chumbani na mwathirika wa tukio. "Pasipokujua kwamba mgeni huyo ambaye mwathiriwa wa tukio anamwita binamu, ana nia ovu, alimvua nguo za ndani kisha kumlaza kitandani na kuanza kumbaka.

"Baada ya kufikishwa kituo cha polisi, mshtakiwa alihojiwa na kukiri kutenda kosa hilo ambapo alidai kwamba mtoto huyo ni mtu wa sita katika idadi ya wanawake aliokwisha kuwabaka kwa nyakati tofauti," Erasto alidai.

Pia, baada ya kupandishwa kizimbani, mshtakiwa alikiri kufanya ubakaji huo huku akiomba mahakama hiyo kumpunguzia adhabu ya kifungo, akiahidi kutorudia tena kwa madai kwamba anajutia kutenda ukatili huo. Licha ya utetezi huo, mahakama hiyo ilitoa adhabu ya kifungo cha maisha jela kutokana na kile kilichoelezwa na Hakimu Kagimbo kuwa kosa hilo halina adhabu mbadala linapotendeka kwa mtoto mwenye umri chini ya miaka 10.

Hukumu ya kifungo cha maisha ni ya tatu kutolewa na mahakama ya wilaya hiyo katika kipindi cha miezi minne tangu kuanza kwa shughuli za mahakama kwa mwaka 2020.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, akitoa maelekezo kwa Mkuu wa Wilaya ya Chamwino, Vumila Nyamoga, wakati wa ziara yake ya kukagua ujenzi wa Hospitali ya wilaya hiyo inayojengwa katika kijiji cha Mlowa, mkoani Dodoma jana. **PICHA: PAUL MABEJA**

## Ahojiwa tuhuma za kuibiwa silaha

**Na Ndalike Sonda,** KAHAMA

JESHI la Polisi mkoani Shinyanga linamhoji mkazi wa Mbulu wilayani Kahama, Renatus Maji (44) kwa tuhuma za uzembe wa kuibiwa silaha yenye risasi 12 ikiwa ndani ya gari.

Kwa Mujibu wa taarifa ya Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Debora Magiligimba, tukio hilo lilitokea Aprili 20, saa nne usiku katika mtaa wa Phantom mjini Kahama na kutaja silaha iliyoibiwa kuwa ni bastola.

Kamanda Magiligimba alisema silaha hiyo ilikuwa imehifadhiwa kwenye gari lake alilokuwa ameliacha nje ya hoteli moja eneo hilo.

Alisema wezi hao walivunja kioo cha mlango wa abiria na kuiiba pamoja na fedha taslimu Sh. 600,000.

Kamanda Magiligimba alisema walifanya msako ukihusisha taarifa za kiitelijensia na kufanikiwa kuipata silaha hiyo ikiwa imetelekezwa karibu na Kituo cha Polisi Kahama na juhudi za kuwatafuta watuhumiwa hao zinaendelea.

"Renatus aliibiwa silaha yake pistol ikiwa na risasi 12 na watu ambao hawajafahamika, silaha hiyo alikuwa ameifungia kwenye dashboard ndani ya gari lake alilokuwa ameliacha nje ya hoteli wakati akiwa anakula chakula," alisema Magiligimba.

"Mbinu iliyotumika ni kuvunja kioo kidogo cha abiria upande wa kulia na kuingia ndani ya gari hilo kisha kuiba silaha hiyo pamoja na pesa taslimu Sh. 600,000 bila yeye mmiliki kujua," alisema Kamanda Magiligimba.

Alisema wanaendelea kumhoji mmiliki wa silaha hiyo kutokana na uzembe wa kushindwa kuzingatia masharti ya umiliki wa silaha na kutoa wito kwa wamiliki wa silaha kufuata masharti ya umiliki.

# Wabobezi 14 wa Sekta Binafsi kuifuatilia corona

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA hatua inayoonyesha kukabiliana na kuenea kwa maambukizi ya ugonjwa wa corona sambamba na kutathmini athari kiuchumi katika kongani zake, Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), imeunda kamati ya ushauri yenye wajumbe 14.

Taasisi hiyo imesema watu hao ni waliobobea kwenye sekta mbalimbali.

Mwenyekiti wa TPSF, Angelina Ngalula, alisema kamati imepewa majukumu makuu manne ikiwamo kutoa ushauri halisia kuhusu athari zitakazotokana na Covid-19 kwenye kongani zote za sekta binafsi.

"Tunategemea kamati itatoa ushauri na mapendekezo yenye mashiko kwa serikali, taasisi za kifedha na mashirika mbalimbali ya kikanda na kimataifa kuhusu namna bora ya kujenga na miradi ambayo imeathirika kutokana na Covid-19," alisema Ngalula ambaye aliambatana na

Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Biashara (TNBC), Dk. Godwill Wanga.

Alisema kamati ambayo imejumuisha wasomi na wataalamu wazoefu na waliobobea watatoa ushauri wa mikakati ya uwekezaji na kusaidia viwanda vinavyozalisha bidhaa zinazopelekwa nje ya nchi.

Alisema kamati hiyo itatoa mapendekezo ya kisera kwa serikali namna bora ya kukabiliana na madhara yatakayokuwa yameletwa na Covid-19.

Aliwataja wajumbe hao ni Dk. Hoseana Lunogelo, Dk.Tausi Kida, Lawrence Mafuru, Phillip Redman, Dk. Charles

Kimei, Susan Mashibe, Dk. Joyce Mapunjo. Kwa mujibu wa Ngalula, wengine ni Michal Bacham, Geoffrey Kirenga, . Jennifer Bash, John Ulanga, Edwin Bruno, Seif Said Seif na Aloys Bahebe.

Dk. Wanga mbali ya kupongeza uteuzi wa kamati hiyo mahiri, alitaka kampuni kutotumia mwanya wa ugonjwa wa corona kutolipa kodi kwani zipo sekta nyingine bado zinafanya vizuri katika uzalishaji.

Dk. Wanga alizihamasisha kampuni ziendelee na kuzalisha kwani serikali inaendelea kuchukua hatua stahiki kukabiliana na kuenea kwa maambukizi ya ugonjwa wa corona nchini.

# BANK OF BARODA (TANZANIA) LTD.

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uonyeshaji ya Mwaka 2014)**

## WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31.03.2020

(Kiasi kwa shilingi milion)

| | | ROBO MWAKA YA SASA | ROBO MWAKA ILIYOPITA 31.12.2019 |
|---|---|---|---|
| A. | MALI | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 4,492 | 2,955 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 11,542 | 21,842 |
| 3 | Uwekezaji katika Amana za Serikali | 24,106 | 21,172 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 30,095 | 32,749 |
| 5 | Hundi na Mihamala ya Kushughulikiwa | 44 | - |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo iliyotolewa kwa Benki Nyingine | - | - |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 102,406 | 113,652 |
| 12 | Mali Nyingine | 3,823 | 3,378 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 1,301 | 1,349 |
| 16 | **Jumla ya Mali** | **177,809** | **197,097** |
| B. | DHIMA | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 3,561 | 5,847 |
| 18 | Amana za Wateja | 131,601 | 149,691 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 125 | 183 |
| 23 | Limbikizo la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 80 | 38 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Mihamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 39 | 36 |
| 27 | Dhima Nyingine | 1,979 | 1,898 |
| 28 | Madeni | - | - |
| 29 | **JUMLA YA DHIMA** | **137,385** | **157,693** |
| 30 | **MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **40,424** | **39,404** |
| C. | FEDHA ZA WANAHISA | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 10,000 | 10,000 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | - | - |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 28,236 | 27,277 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 1,020 | 1,103 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 1,168 | 1,024 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| 37 | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **40,424** | **39,404** |
| 38 | Dhima zisizo Dhahiri | 11,202 | 12,413 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 2,435 | 2,495 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 1,167 | 893 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| D | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 23% | 20% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 2% | 2% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 77% | 74% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali | 58% | 58% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 88% | 85% |
| (vi | Ongezeko la Amana | -13% | 17% |
| (vii | Ongezeko la Mali | -10% | 14% |

## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 MACHI 2020

(Kiasi kwa shilingi milion)

| | | ROBO YA MWAKA SASA 31.03.2020 | ROBO YA MWAKA LINGANISHI 31.03.2019 | LIMBIKIZO LA MWAKA WA SASA 31.03.2020 | LIMBIKIZO LA MWAKA LINGANISHI 31.03.2019 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 3,732 | 3,498 | 3,732 | 3,498 |
| 2 | Gharama za Riba | 1,289 | 1,109 | 1,289 | 1,109 |
| 3 | **Mapato halisi ya Riba (1 kutoa 2)** | **2,443** | **2,389** | **2,443** | **2,389** |
| 4 | Madeni Viza yaliyofutwa | 34 | - | 34 | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 274 | 210 | 274 | 210 |
| 6 | **Mapato yasiyo ya Riba:** | **292** | **369** | **292** | **369** |
| | 6.1 Faida/Hasara zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 105 | 167 | 105 | 167 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 186 | 201 | 186 | 201 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 0 | 1 | 0 | 1 |
| 7 | **Gharama Zisizo na Riba:** | **1,205** | **1,173** | **1,205** | **1,173** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | 543 | 578 | 543 | 578 |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | 105 | 16 | 105 | 16 |
| | 7.3 Gharama Nyingine | 558 | 579 | 558 | 579 |
| | 7.4 Other Provision | - | - | - | - |
| 8 | **Faida/(Hasara) ya Uendeshaji** | **1,222** | **1,375** | **1,222** | **1,375** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | 201 | 366 | 201 | 366 |
| 10 | **Faida/(Hasara) ya Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **1,020** | **1,009** | **1,020** | **1,009** |
| 11 | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainishi)** | - | - | - | - |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **1,020** | **1,009** | **1,020** | **1,009** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | **50** | **48** | **50** | **48** |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 102 | 101 | 102 | 101 |
| 15 | **Idadi ya Matawi** | 4 | **4** | **4** | **4** |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 2% | 2% | 2% | 2% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 10% | 10% | 10% | 10% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 44% | 43% | 44% | 43% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 6% | 6% | 6% | 6% |

## TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO ILIYOISHIA 31.03.2020

(Kiasi kwa shilingi milion)

| | | ROBO YA MWAKA YA SASA 31.03.2020 | ROBO YA MWAKA ILIYOPITA 31.12.2019 | LIMBIKIZO LA MWAKA WA SASA 31.03.2020 | LIMBIKIZO LA MWAKA LINGANISHI 31.03.2019 |
|---|---|---|---|---|---|
| I | Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | 1,222 | 563 | 1,222 | 1,375 |
| | Marekebisho kwa ajili ya: | - | - | - | - |
| | -Hasara katika Mali | 330 | 1,150 | 330 | 260 |
| | -Prior Period Adjustment | - | (344) | - | - |
| | -Badiliko Halisi Katika Mikopo | 10,972 | (12,718) | 10,972 | (222) |
| | -Faida/Hasara kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Amana | (18,091) | 9,108 | (18,091) | 2,728 |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (2,217) | 150 | (2,217) | 215 |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 267 | 10,287 | 267 | 4,902 |
| | -Kodi Iliyolipwa | (201) | (366) | (201) | (366) |
| | *-Mengineyo (Bainisha)* | - | (911) | - | (912) |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa(tumika) kwa Shughuli za Uendeshaji** | **(7,718)** | **6,919** | **(7,718)** | **7,980** |
| II | Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji: | | | | |
| | -Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| | -Ununuzi wa Mali za Kudumu | (9) | (17) | (9) | (13) |
| | -Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| | -Ununuzi wa Amana zisizoshughulikiwa na Mawakala | (2,935) | 8,181 | (2,935) | (5,029) |
| | -Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | *-Mengineyo (ainisha)* | - | - | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa(zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(2,943)** | **8,164** | **(2,943)** | **(5,041)** |
| III | Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli Kifedha: | | | | |
| | -Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | -Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | -Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| | -Gawio Lililolipwa kwa Fedha Tasilimu | - | - | - | - |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| | *-Mengineyo (Bainisha)* | - | - | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) Kwa Shughuli za Kifedha** | **-** | **-** | **-** | **-** |
| IV | Fedha tasilimu na Mali Zinazofanana na Fedha Tasilimu: | | | | |
| | -Ongezeko/ punguzo Halisi Katika Fedha Tasilimu na Mali Zinazofanana na Fedha Tasilimu | **(10,661)** | **15,083** | **(10,661)** | **2,938** |
| | -Fedha Tasilimu na Mali zinazofanana na Fedha Tasilimu Mwanzoni mwa Robo/Mwaka | 45,898 | 30,815 | 45,898 | 31,307 |
| | -Fedha Tasilimu na Mali zinazofanana na Fedha Tasilimu Mwanzoni mwa Robo/Mwaka | **35,237** | **45,898** | **35,237** | **34,245** |

## TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 MACHI 2020

(Kiasi kwa shilingi milion)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo Juu ya Bei ya Hisa | Mapato yaliyo Bakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineya (Bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **MWAKA WA SASA** | | | | | | | |
| **Salio la Mwanzo wa Mwaka** | **10,000** | **-** | **28,381** | **775** | **-** | **249** | **39,404** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 1,020 | - | - | - | 1,020 |
| Mapato Mengineyo yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (144) | 144 | - | - | - |
| Tengo la ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la Mwisho wa Mwaka** | **10,000** | **-** | **29,257** | **919** | **-** | **249** | **40,424** |
| **MWAKA ULIOPITA** | | | | | | | |
| **Salio la Mwanzo wa Mwaka** | **10,000** | **-** | **24,134** | **3,984** | **937** | **-** | **39,055** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 1,103 | - | - | - | 1,103 |
| Mapato Mengineyo yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 3,209 | (3,209) | - | - | - |
| Tengo la ziada ya Jumla | - | - | 937 | - | (937) | - | - |
| Mengineyo | - | - | (1,002) | - | - | - | (1,002) |
| | - | - | - | - | - | 249 | 249 |
| **Salio la Mwisho wa Mwaka** | **10,000** | **-** | **28,381** | **775** | **-** | **249** | **39,404** |

**BAADHI YA MAELEKEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31.03.2020**

**Katika Kuandaa taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za Mwaka uliopita. (Mabadiliko katika sera za uandaaji wa taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya /mwaka wa sasa, yaelezwe kwa mujibu wa ISA 34 na ISA 8)**

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Rajendra Sadashiv Mohrir (Mkurugenzi Mtendaji) | | 16th April, 2020 |
| Deogratias Edward Ndushi Mkuu wa Fedha | | 16th April, 2020 |
| Mwita Mohamed Mwita (Mkaguzi wa Ndani) | | 16th April, 2020 |

**Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya Kimataifa vya Uwasirishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya Mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.**

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Dkt. Proches Meshili Kiwango Ngatuni | | 16th April, 2020 |
| Dkt. Imanueli Daniel Mnzava | | 16th April, 2020 |

BancABC part of atlasmara

# AFRICAN BANKING CORPORATION TANZANIA LIMITED

# UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

## IMETOLEWA CHINI YA KANUNI YA 7 NA YA 8 YA KANUNI ZA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA (UONESHAJI) YA MWAKA 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 MACHI 2020

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya /Mwaka wa sasa 31-Mar-20 | Robo Mwaka/Mwaka uliopita 31-Dec-19 |
|---|---|---|---|
| **A** | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 3,522 | 3,572 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 11,307 | 12,790 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 33,333 | 33,052 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 2,922 | 2,288 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 102,996 | 95,550 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 126,880 | 127,755 |
| | | - | - |
| 12 | Mali Nyingine | 32,390 | 26,548 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 1,000 | 1,000 |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 3,583 | 6,639 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **317,933** | **309,194** |
| **B** | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 97,144 | 92,642 |
| 18 | Amana za Wateja | 100,589 | 99,021 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | - | - |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | - | - |
| 27 | Dhima Nyingine | 6,150 | 4,356 |
| 28 | Madeni | 71,060 | 69,553 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **274,943** | **265,571** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **42,990** | **43,623** |
| **C** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 122,954 | 122,954 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 1,195 | 1,195 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (80,526) | (71,756) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | (633) | (8,769) |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | - | - |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **42,990** | **43,623** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 3,493 | 3,137 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 19,691 | 17,957 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 15,750 | 15,351 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| **D** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (I) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 13.52% | 14.11% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 13.81% | 12.55% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 72.13% | 74.67% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 39.91% | 41.32% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 83.71% | 83.65% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 3.17% | -4.18% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 2.83% | -3.56% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 MACHI 2020

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka sasa 31-Mar-20 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita 31-Mar-19 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31-Mar-20 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 31-Mar-19 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 10,245 | 10,423 | 10,245 | 10,423 |
| 2 | Gharama za Riba | (4,751) | (4,774) | (4,751) | (4,774) |
| **3** | **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **5,494** | **5,649** | **5,494** | **5,649** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 182 | (735) | 182 | (735) |
| **6** | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **1,073** | **1,856** | **1,073** | **1,856** |
| 6.1 | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 479 | 466 | 479 | 512 |
| 6.2 | 6.2 Ada na Kamisheni | 180 | 210 | 180 | 165 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.3 | 6.4 Mapato Mengine | 413 | 1,179 | 413 | 1,179 |
| **7** | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(7,348)** | **(7,978)** | **(7,348)** | **(7,978)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (2,536) | (2,535) | (2,536) | (2,535) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | - | - | - | - |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (4,812) | (5,443) | (4,812) | (5,443) |
| **8** | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **(599)** | **(1,209)** | **(599)** | **(1,209)** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (34) | - | - | - |
| **10** | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **(633)** | **(1,255)** | **(633)** | **(1,255)** |
| 11 | Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | - | - | - | - |
| **12** | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **(633)** | **(1,255)** | **(633)** | **(1,255)** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 151 | 161 | 151 | 161 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | (0.26) | (0.13) | (0.06) | (0) |
| 15 | Mapato yaliyopatikana kwa Kushiriki | - | - | - | - |
| 16 | Idadi ya Matawi | 7 | 7 | 7 | 7 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | 0 | - | 0 | - |
| (I) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | -0.81% | -0.39% | -0.81% | -0.39% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | -5.85% | -2.40% | -5.85% | -2.40% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 111.90% | 106.32% | 111.90% | 106.32% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 3.37% | 0.78% | 3.37% | 0.78% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 31 MACHI 2020

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya sasa 31-Mar-20 | Robo Mwaka iliyopita 31-Dec-19 |
|---|---|---|---|
| **I** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | (599) | (8,624) |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | - | - |
| | - Hasara Katika Mali | 1,834 | 9,515 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | 876 | 10,351 |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 6,071 | (8,357) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - 281 | 7,558 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 3,301 | (17,053) |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (5,842) | (1,551) |
| | - Kodi Iliyolipwa | (34) | (198) |
| | - Mengineyo (bainisha) | - | 927 |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **5,325** | **(7,431)** |
| **II** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | - | - |
| | Gawio Lililopokewa | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (82) | (3,540) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(82)** | **(3,540)** |
| **III** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | 6,940 |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **-** | **6,940** |
| | | - | - |
| **IV** | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | - | - |
| | Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | 5,242 | (4,031) |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 115,504 | 119,535 |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka** | **120,747** | **115,504** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 MACHI 2020

(Kiasi kwa shilingi millioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | 122,954 | - | (80,525) | 130 | 0 | 1,065 | 43,624 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (633) | - | - | - | (633) |
| Hisa za upendeleo | - | | | | | | |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | 122,954 | - | (81,158) | 130 | 0 | 1,065 | 42,991 |
| | - | - | - | - | - | - | - |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | 116,014 | - | (72,910) | 0.22 | 1,284 | 1,065 | 45,453 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (8,769) | - | - | - | (8,769) |
| Hisa za upendeleo | 6,940 | - | - | - | - | - | |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (130) | 130 | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | 1,284 | - | (1,284) | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | 122,954 | - | (80,525) | 130 | 0 | 1,065 | 43,624 |

| | Jina | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|---|
| Ofisa Mtendaji Mkuu | I. John | | 24th April 2020 |
| Mkuu wa Fedha | H. Kharbush | | 24th April 2020 |
| Mkaguzi Mkuu wa Ndani | J. Kilato | | 24th April 2020 |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi

| | Jina | Sahihi | Tarehe |
|---|---|---|---|
| 1 Mkurugenzi | P. Ishengoma | | 24th April 2020 |
| 2 Mkurugenzi | Mr.R. Dave | | 24th April 2020 |

215713901

# TANGAZO

BancABC part of atlasmara

## AFRICAN BANKING CORPORATION TANZANIA LIMITED

## MINIMUM DISCLOSURES OF BANK CHARGES AND FEES

| | PRICING (TZS) | PRICING (US $ / EUR) | PRICING (GBP) |
|---|---|---|---|
| **PERSONAL BANKING** | | | |
| **SAVINGS ACCOUNT** | | | |
| **FAHARI** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 10,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 10,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 50,000.00 | $ 100.00 | £ 100.00 |
| Monthly Service Fee | Free | Free | Free |
| | | | |
| **MWANGAZA JUNIOR ACCOUNT** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 20,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 20,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 20,000.00 | $ 500.00 | £ 500.00 |
| Monthly Service Fee (1 free w/drawal per quarter) | Free | Free | Free |
| Extra fee for more than 1 w/drawal per quarter | TZS 1,500.00 | $ 2.00 | £ 2.00 |
| | | | |
| **WEKEZA SAVINGS ACCOUNT (BALANCE BUILD UP)** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | N/A |
| Opening balance | Free | Free | N/A |
| Minimum Operating Balance | NIL | NIL | N/A |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 50,000.00 | $ 25.00 | N/A |
| Monthly Service Fee* | Free | Free | N/A |
| | | | |
| CURRENT ACCOUNT | | | |
| **AMANA** | | | |
| Account Opening Fee | Free | N/A | N/A |
| Opening balance | TZS 20,000.00 | N/A | N/A |
| Minimum Operating Balance | TZS 3,000.00 | N/A | N/A |
| Minimum Interest Bearing Balance | N/A | N/A | N/A |
| Monthly Service Fee* | TZS 2,000.00 | N/A | N/A |
| | | | |
| **MARIDHAWA** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | N/A |
| Opening balance | TZS 25,000.00 | $ 25.00 | N/A |
| Minimum Operating Balance | TZS 6,000.00 | $ 5.00 | N/A |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 2,000,000.00 | $ 2,000.00 | N/A |
| Monthly Service Fee* | TZS 5,000.00 | $ 10.00 | N/A |
| | | | |
| **PREMIUM** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 35,000.00 | $ 30.00 | £ 30.00 |
| Minimum Operating Balance | NIL | NIL | NIL |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 3,000,000.00 | $ 3,000.00 | £ 3,000.00 |
| Monthly Service Fee* | TZS 10,000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| | | | |
| **SME BANKING** | | | |
| **AMANA BIZ ACCOUNTS** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 100,000.00 | $ 100.00 | £ 100.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 1,000,000.00 | $ 1,000.00 | £ 1,000.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | TZS 5,000,000.00 | $ 5,000.00 | £ 5,000.00 |
| Monthly Service Fee* | TZS 20,000.00 | $ 15.00 | £ 15.00 |
| | | | |
| **CORPORATE BANKING** | | | |
| **CORPORATE CURRENT ACCOUNTS** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 500,000.00 | $ 250.00 | £ 250.00 |
| Minimum Operating Balance | NIL | NIL | NIL |
| Minimum Interest Bearing Balance | NIL | NIL | NIL |
| Monthly Service Fee* | TZS 25,000.00 | $ 20.00 | £ 15.00 |
| | | | |
| **CORPORATE CALL ACCOUNTS** | | | |
| Account Opening Fee | Free | Free | Free |
| Opening balance | TZS 10,000,000.00 | $ 10,000.00 | £ 10,000.00 |
| Minimum Operating Balance | TZS 10,000,000.00 | $ 10,000.00 | £ 10,000.00 |
| Minimum Interest Bearing Balance | NIL | NIL | NIL |
| Monthly Service Fee* | TZS 25,000.00 | $ 20.00 | £ 15.00 |
| | | | |
| **GENERAL CHARGES** | | | |
| Bankers Cheque | TZS 50,000.00 | $ 25.00 | N/A |
| | | | |
| DISHONORED/UNPAID CHEQUE | | | |
| Fund related | TZS 120,000.00 | $ 120.00 | N/A |
| Technical | TZS 60,000.00 | $ 60.00 | N/A |
| | | | |
| **Cheque book Processing Fee:** | | | |
| 25 leaves | TZS 15,000.00 | $ 15.00 | £ 15.00 |
| 50 leaves | TZS 30,000.00 | $ 30.00 | £ 30.00 |
| 100 leaves | TZS 60,000.00 | $ 60.00 | £ 60.00 |
| Uncollected cheque book after 3 months | TZS 15,000.00 | $ 15.00 | £ 15.00 |
| 3rd party encashment (with 3rd party indemnity) | TZS 25,000.00 | 10% Per Cheque | 10% Per Cheque |
| **Stop Payment Charges** | TZS 60,000.00 | $ 60.00 | £ 50.00 |
| | | | |
| **TRANSACTIONAL SERVICE FEES** | | | |
| **With banks via Standing Orders** | | | |
| Standing Order - internal same customer ( set up fee - once off) | TZS 10,000.00 | $ 5.00 | £ 5.00 |
| Standing Order - internal other customers ( per transaction) | TZS 4,000.00 | $ 3.00 | £ 2.00 |
| Standing Order - Other local bank | TZS 40,000.00 | $ 30.00 | £ 20.00 |
| Amendment | TZS 5,000.00 | $ 5.00 | £ 5.00 |
| | | | |
| **DEPOSIT/WITHDRAWAL TRANSACTIONS:** | | | |
| - Cash Deposit at Branch | Free | Free | Free |
| - Cash Deposit at Branch small denominations 500 above 50 | 0.3% Min 1,000 | 3% On Small denominations | N/A |
| - Cash Deposit at Branch small denominations (2,000 and be | 0.3% Min 1,000 | 3% On Small denominations | N/A |
| - Cash Deposit at Branch coins above 100,000 | 0.3% Min 1,000 | N/A | N/A |
| With Account Transfers (Internal) | N/A | N/A | N/A |
| - Cheque deposit | Free | Free | Free |
| - Cash withdrawal Personal Banking ( over the counter) up to | TZS 2,500.00 | 1% Min 10 | 1% min 10 |
| - Cash withdrawal Personal Banking ( over the counter) btn 5 | TZS 6,000.00 | 1% Min 10 | 1% min 10 |
| - Cash withdrawal Personal Banking ( over the counter) abov | 0.15% MAX 200,000 | 1% Min 10 | 1% min 10 |
| - Cash withdrawal SME ( over the counter) | 0.15%Min 3000 Max 200000 | 1% Min 10 | 1% min 10 |
| - Cash withdrawal Corporate Banking | 0.15%Min 7,500 Max 200,000 | 1% Min 10 | 1% min 10 |
| - Deposit charges - Financial Institution. | Free | Free | Free |
| - Deposit charges - Financial Institution - small denominations | Free | 2%On small denominations* | 2%On small denominations* |
| | | | |
| Account Closure | TZS 10,000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| Dormant Account Reactivation | TZS 10,000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| Dormant Account monthly fee | TZS 10,000.00 | $ 10.00 | £ 10.00 |
| Premature/cancellation fixed deposit fee | 50% Accrued Interest is Forfeited. Breaking 1st month all interest forfeited | 50% Accrued Interest is Forfeited. Breaking 1st month all interest forfeited | 50% Accrued Interest is Forfeited. Breaking 1st month all interest forfeited |
| Monthly statements | Free | Free | Free |
| Interim Statements (per page) | TZS 5,000.00 | $ 3.00 | £ 3.00 |
| Search fee documents (after 3 months) | TZS 80,000.00 | $ 40.00 | £ 40.00 |
| Audit confirmation | TZS 75,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Balance Certificate | TZS 75,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Reference Letter | TZS 75,000.00 | $ 50.00 | £ 50.00 |
| Inter Account Transfers | Free | Free | Free |
| T T Outward local - TISS | TZS 10,000.00 | $ 10.00 | N/A |
| T T Outward local - EFT | TZS 3,000.00 | N/A | N/A |
| T T Inward local TISS | Free | Free | N/A |
| Salary processing (per entry) | TZS 1,000.00 | $ 1.00 | £ 1.00 |
| International Outward T T | N/A | Comm 0.25% Min 50 Max 500 | comm 0.25% min 50 max 350 |
| International Inward T T | N/A | Free | Free |
| Travellers Chq. Deposit | N/A | N/A | N/A |
| Foreign BankDrafts | N/A | $ 50.00 | £ 30.00 |
| Outward Cheque for Collection | N/A | N/A | N/A |
| Outward Bills for collection | N/A | 0.25% min 50 + $ 50 (courier charge) | 0.25% min 50 + $ 50 (courier charge) |
| Inward Bills for Collection | N/A | 0.25% MIN 50 | 0.25% MIN 50 |
| Advising fee (Inward Bill & LCs ) | N/A | $ 200.00 | £ 200.00 |
| Travellers Chq. (Issue) | N/A | N/A | N/A |
| Letters of Credit | N/A | 1% per qtr + $ 50 (total min $250) | 1% per qtr + $ 50 (total min $250) |
| Bank Guarantees | 1% Per Qtr Min $ 200 | 1% per qtr min $200 | 1% per qtr min $200 |

ewura
Energy and Water Utilities Regulatory Authority
ISO 9001:2015 Certified

MAKAO MAKUU
Ghorofa ya 4, Jengo la PSSSF, Barabara ya Makole
S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania
Simu: +255-26 2329002-3; Nukushi: +255-26 2329005
Barua pepe: info@ewura.go.tz Tovuti: http://www.ewura.go.tz

## TAARIFA KWA UMMA

## JUU YA UUZAJI WA MAFUTA YA PETROLI KIHOLELA KUTUMIA MAGARI MADOGO

Katika siku za hivi karibuni, kumekuwapo na ushamiri wa uuzwaji mafuta hasa ya Petroli na Dizeli katika maeneo yasiyoruhusiwa (nje ya vituo vya mafuta) pasipo kuzingatia masuala ya usalama na mazingira ( Health, Safety and Environment) katika jiji la Dar es Salaam.

Wauzaji hawa wa mafuta wamekuwa wakitumia magari madogo yasiyoruhusiwa kubeba mafuta na kuwauzia wenye magari ya mizigo nje ya vituo vya mafuta hususan majumbani, kwenye yadi za kupaki magari, stendi za mabasi na pembezoni mwa barabara.

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji(EWURA) inapenda kutoa tahadhari kwamba uuzaji wa mafuta kwa namna hii ni hatari kwa ssalama wa watu na mali, afya za wahusika na mazingira. Aidha, uuzaji huo wa kiholela wa mafuta ni kinyume cha Sheria, kanuni na taratibu za nchi. Pia, ubora wa mafuta haya hauwezi kuhakikiwa na mara nyingi mafuta haya huwa hayakidhi viwango stahiki vya ubora; hivyo wanunuaji wa mafuta hayo wanahatarisha vyombo vyao na kusababisha uharibifu na gharama kubwa za matengenezo ya magari.

Kwa mujibu wa kifungu cha 131 cha Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015, mtu yeyote anayetaka kufanya biashara ya mafuta, sharti aombe na apate leseni kutoka EWURA. Kufanya biashara ya kuuza mafuta bila leseni ya EWURA, adhabu yake ni faini ya **shillingi million 20** au kifungo kisichopungua **miaka miwili** na kisichozidi **miaka mitano** au vyote kwa pamoja.

EWURA inatoa **ONYO** kali kwa wote wanaojihusisha na uuzaji huu wa mafuta kiholela kuacha mara moja. Ukaguzi umeanza kufanyika katika jiji la Dar es Salaam, kwa kuhusisha pia vyombo vya usalama ili kubaini uovu huu na hatua kali zitachukuliwa kwa mujibu wa Sheria.

**Imetolewa na**
**MKURUGENZI MKUU**
**22 Aprili, 2020**

ewura
Energy and Water Utilities Regulatory Authority
ISO 9001:2015 Certified

MAKAO MAKUU
Ghorofa ya 4, Jengo la PSSSF, Barabara ya Makole
S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania
Simu: +255-26 2329002-3; Nukushi: +255-26 2329005
Barua pepe: info@ewura.go.tz Tovuti: http://www.ewura.go.tz

## TAARIFA KWA UMMA

## UFAFANUZI KUHUSU KUSHUKA BEI ZA MAFUTA

Katika siku za hivi karibuni, kumekuwepo na taarifa katika mitandao ya kijamii kuhusu kushuka kwa bei ya mafuta ghafi nchini Marekani, hali iliyosababisha watu kuanza kuhoji kwanini bei za mafuta hapa nchini hazishuki kwa kiwango kinachoonekana kushuka katika solo la Marekani.

Bei za mafuta nchini Marekani zinazotangazwa kupungua kwa kiwango kikubwa ni zile za mafuta ghafi (crude oil) na siyo mafuta yaliyosafishwa (refined petroleum products). Punguzo hili la bei linatokana na kukosa mahali pa kuhifadhia mafuta hayo nchini Marekani.

Vilevile, kwa taratibu zilizopo, mafuta yanaingizwa nchini na mshindi wa zabuni za uagizaji mafuta kwa pamoja, ambapo kwa kiasi kikubwa; mafuta yanayoletwa nchini hutokea nchi za **Uarabun**i. Hivyo basi, kushuka kwa bei za mafuta Marekani kunaweza kusilete unafuu katika soko la Tanzania, kwa kuwa mafuta yetu yananunuliwa Uarabuni.

Ikiwa mafuta hayo yatashuka katika Soko la Dunia **(Uarabuni)**, itachukua kipindi cha **miezi miwili (2)** ndipo Watanzania waone faida katika bei zinazotolewa na EWURA kila Jumatano ya kwanza ya mwezi husika.

Kanuni zinazosimamia biashara ya mafuta zinamtaka kila mfanyabiashara wa mafuta kwa jumla awe na hifadhi ya mafuta kwa muda wa siku zisizopungua 15 kulingana na hisa zake katika soko. Wafanyabiashara wote hususan wa jumla wanatakiwa kuzingatia Sheria, kanuni na taratibu zilizopo katika kuendesha biashara ya mafuta

Katika kuboresha uhifadhi na upatikanaji wa mafuta nchini *(Security of supply),* Serikali kupitia Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) na Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC), inafanya mchakato wa kujenga maghala ya kuhifadhi mafuta nchini.

EWURA inaendelea kufuatilia kwa karibu mwenendo wa soko la dunia kwa ujumla ili kuhakikisha kwamba Tanzania inanufaika na manufaa yoyote yanayoweza kupatikana kutokana na mabadiliko ya mwenendo wa soko la mafuta katika maeneo ambayo huagiza mafuta kwa matumizi ya ndani.

**Imetolewa na:**
**MKURUGENZI MKUU**
**22 Aprili, 2020**

## JANGA LA MIKOPO...

# Walimu wanavyokopa kupitiliza, kisha kukimbia vituo vya kazi

- DAS aonya 'angalieni, fuateni hivi'

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

KUNA kilio cha kushuka kiwango cha elimu katika shule wilayani hapa na tayari sababu inaelekezwa kwenye tija ya walimu. Inadaiwa sehemu kubwa wanakimbia vituo vya kazi, kwa mikasa ya madeni kutokana na mikopo wanayojibebesha kutoa taasisi za kifedha.

Inadaiwa pesa wanazopata hazifanani na kile wanachokopa na pindi wanaelemewa, uamuzi wa mwisho wao ni kukimbia madeni hayo ya kifedha.

Kimsingi, mtumishi wa umma anatakiwa kuingia kwenye mikopo kisheria unaomkata theluthi moja ya mshahara wake, lakini wengi hujikuta wamekopa zaidi zisizoendana na kiwango cha mshahara wa mwezi.

Inaelezwa, kinachotokea walimu wa shule za msingi na sekondari wanaingia kwenye mkopo na benki na baadaye wanaingia tena kwenye mkopo na taasisi za ukopeshaji mitaani na wanaacha kadi zao za benki mahali, huku wanachokopa hakiingii katika maendeleo, kinyume na malengo ya taasisi za kifedha.



Mwenyekiti wa Chama cha Walimu Tanzania Ushetu, Mwalimu Juma Nyakanyenge, alipozungumza na wajumbe wa mkutano wa chama hicho, baada ya kuchaguliwa kukiongoza chama, hivi karibuni. **PICHA ZOTE: SHABAN NJIA.**

**DAS KAHAMA**

Katibu Tawala wa Wilaya ya Kahama, Timothy Ndanya, ameuambia mkutano wa Chama cha Walimu Wilaya ya Ushetu, kuwa na nidhamu ya fedha wanazozipata na kutojihusisha na mikopo isiyofaa.

Anasema, walimu wanakopa kiwango kikubwa kisichoendana na mshahara yao, hata kufikia hatua ya kukabidhi kadi zao za benki kwa taasisi za mikopo mitaani, kufikia kukimbia vituo vyao vya kazi, baada ya kushindwa kumudu marejesho.

Ndanya anasema, Halmashauri ya Wilaya Ushetu ina upungufu wa walimu, waliopo ni 1,025 sawa na asilimia 58 na wanaohitajiwa wako 749, kutoka jumla ya 1,774.

**MIKOPO WALIMU.**

Timoth Ndanya, anasema utoro unaotokana na mkopo hiyo umesababisha wanafunzi kukosa masomo na kushindwa kufanya vyema kwenye mitihani yao ya mwisho.

Ndanya anasema, kila mwalimu anayehitaji mkopo anatakiwa kukopa moja ya tatu ya mshahara wake kutoka taasisi za kifedha zinazotambulika kisheria na sio kukopa mitaani, ambazo hazitambuliki kisheria.

"Mikopo hii mnayoingia walimu inawafanya mnakimbia vituo vyenu vya kazi. Mnaingia kwenye mikopo mikubwa ambayo haiendani na kiwango cha mshahara yenu na kujikuta mwisho wa siku mnapokea Sh. 60,000 hadi Sh.100,000 fedha ambayo haiwezi kukusaidia chochote ndani ya mwezi," anatahadharisha Ndanya.

"Walimu nchi nzima hawatoshi kwenye shule zetu, lakini inatulazimu kumfukuza mwalimu kazi, endapo anakwenda kinyume na maadili ya utumishi wa umma," anaendelea.

Ndanya anatumia fursa hiyo kuwataka walimu wajiendeleze kiuchumi hasa katika shughuli za kilimo cha tumbaku, pamba na mpunga, akiamini kitawasaidia wasiingie sana katika mikopo isiyo ya tija, hata ikawakimbiza vituo vyao vya kazi.

> **"Mikopo hii mnayoingia walimu inawafanya mnakimbia vituo vyenu vya kazi. Mnaingia kwenye mikopo mikubwa ambayo haiendani na kiwango cha mshahara yenu na kujikuta mwisho wa siku mnapokea Sh. 60,000 hadi Sh.100,000 fedha ambayo haiwezi kukusaidia chochote ndani ya mwezi**

**SIASA YA CORONA**

Katibu Tawala Kahama, anaendelea kuwa, baadhi ya walimu wamejikita zaidi kwenye shughuli binafsi, badala ya kufundisha darasani wakiwa vinara wa mabishani hayo, huku wakitelekeza watoto darasani.

Anakumbusha jukumu kuu la mwalimu ni ni kufundisha na kuhakikisha wanafunzi wanafanya vyema masomoni na kwenye mitihani yao ya mwisho, ili kuleta mageuzi ya kuifanya nchi kuwa na vijana wanaojitegemea.

Ndanya anawataka walimu, kupanua darasa la masomo la kuwaelekeza wanafunzi walioko mitaani kila mmoja kwa nafasi yake, namna ya kujikinga na virusi vya ugonjwa wa corona.

"Mitaani kwetu kuna watoto wengi tena wanafunzi wanakaa ki-makundi kwenye michezo yao, hawanawi mikono mara kwa mara, nasi kama walimu ambao tunaishi nao tuhakikishe tunawapatia elimu namna ya kujikinga na ugonjwa huu, ambao kwa sasa uko,: anasema Ndanya.

**UONGOZI CWT**

Mwalimu Juma Nyakanyenge, ni Mwenyekiti wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT), wilayani Ushetu anasema, walimu wengi wanakopa fedha za mikopo na kuzipeleka kwenye anasa, badala ya shughuli za maendeleo au uzalishaji mali kwenye maeneo yao.

Anasema kuwa, ili kuwasaidia wasiendelee kukopa na kukimbia vituo vyao vya kazi, atahakikisha anawatembelea na kuwapatia elimu ya kutumia fursa za mazingira walizonayo kuwekeza kwenye eneo lake, na si kuishia katika mikopo isiyo na tija kila kukichao.

Nyakanyenge anasema, kila mwalimu anayeajiriwa, pia walimu vijana huwa anakutana nao katika Halmashauri ya Ushetu, akimtaka ajipange kimaisha kabla ya kuingia kwenye majukumu mengine yanayoweza yakamsababisha mikopo inayoishia kuwa changamoto asiyomudu.

"Kwenye maeneo yetu ya kazi kuna fursa nyingi ambazo mwalimu anaweza kuzifanya na kujiingiza kipato. Halmashauri ya Ushetu, asilimia kubwa ya wananchi wake wamejikita kwenye kilimo cha tumbaku, pamba, mpunga, dengu, na mpunga na mwalimu anaweza kulima moja ya kilimo hicho," anawamkubusha.

Nyakanyenge anasema Halmashauri ya Ushetu imekuwa ikitoa mikopo kwa vikundi vya ujasiriamali vya vijana, kinamama na wenye ulemavu na walimu wa shule wanapoanzisha kikundi cha uzalishaji mali, wanapata mkopo kupitia Halmashauri wajiinue kimtaji.

Anasema, Ushetu ina frusa nyingi kiuchumi, akitaja kilimo ni mojawapo na kila mwalimu kwenye eneo lake anatumia fursa kujipatia mkopo, hata kumuondoa katika usumbufu wa mikopo yenye riba kubwa, hata baadhi ya walimu wanashindwa kulipa deni.

Mwenyekiti huyo wa CWT, anaahidi kuhakikisha wanaanzisha vikundi vya kukopeshana na kusaidia hilo kufika katika shule nyingi, walimu wakikopeshana, huku akiwasisitiza wanachokopa kisizidi theluthi moja ya pato lao, ambayo ndiyo sheria.

Nyakanyenge anawasisitizia walimu kuwa na nidhamu ya fedha, sambamba na kuwaandalia makazi kabla ya kustaafu, ili fedha watakazopata zitumike kwenye kukuza mtaji na sio ujenzi wa makazi.

Ofisa Utumishi wa Halmashauri ya Ushetu, Manyama Katikiro, katika mkutano wa uchaguzi wa viongozi wa CWT, anawataka wachague viongozi jasiri na wenye uwezo wa kuwakilisha matatizo yao, ambayo kimsingi ni mengi na yanahitaji kutatuliwa mapema.

Katikiro anataja sifa nyingine ya kiongozi stahiki, pasipo kujali itikadi zao, ni kuwa na uwezo wa kutatua changamoto zao watakao kuwa wanaziwasilisha mezani mwao, ili kuhakikisha sekta ya elimu inakuwa kwa maslahi ya wana Ushetu.

Ni mkutano uliomchagua Juma Nyakanyenge, kuwa Mwenyekiti, Thomas Antony (Mweka Hazina), Sanga Maura (Mwakilishi wanawake), Soja Saidi (Mwakilishi Walimu wenye Ulemavu), Basil Petro (Mwakilishi Vijana).

Pia, wawakilishi walimu shule za msingi ni Mayala Mosses, Dotto Pacea, Majani Kulwa, Nyamsusa Robert na Michael Joseph Makoye na wanaowakiksha walimu wa sekondari ni; Makombe Yusuph na Nyalwera Godeliva na Majakiya Moses mwakilishi taasisi.



Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Chama cha Walimu Ushetu, wakimsikiliza mwenyekiti wao (hayupo pichani), baada ya kuchaguliwa.



# Bil. 22.5/- kuwalipa wengine waliopitiwa na reli ya kisasa

**Na Renataha Msungu,** DODOMA

SHIRIKA la Reli Tanzania (TRC), limetenga Sh. bilion 22.5 kwa ajili ya kuwalipa fidia wananchi ambao maeneo yao yamepitiwa na mradi wa ujen zi wa reli ya kisasa (SGR) katika maeneo ya Singida na Dodoma.

TRC imezindua awamu ya pili kwa ajili ya kuwalipa fidia wananchi ambao maeneo yao yatapitiwa na SGR katika mikoa hiyo, na wataanza kulipwa hivi karibuni.

Katika uzinduzi huo uliofanywa na Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Patrobas Katambi, katika Shule ya Sekondari Mkonze jijini hapa, fedha hizo zitalipwa kwa wakazi wa wilaya za Bahi, Dodoma na Manyoni mkoani Singida.

Katambi alisema shirika hilo halitakosea kwa sababu lina majina ya watu wote ambao wanastahili kulipwa haki yao, hivyo atakayejipachika anajisumbua, hawezi kupata fedha yoyote.

"Utaratibu umepangwa wa kueleweka, hivyo wananchi mtulie, kazi ikianza kila mmoja atapata haki yake ya msingi kulingana na eneo alilokuwa nalo," alisema Katambi.

Alisema mara baada ya kukabidhiwa fedha hizo wananchi wanapaswa kujipanga kwa ajili ya kufanya maendeleo na sio starehe kutokana na kuwa watakuwa na fedha za kutosha.

"Nawaomba mkipata fedha mkajenge nyumba, msibweteke kula bata mitaani, mtaumia na mtaziumiza familia zenu zinazowategemea," alisema Katambi.

Meneja msaidizi wa mradi huo kutoka TRC, Mhandisi Christopher Mang'wela, alisema Shirika lake limeshalipa fidia Sh. bilioni 13.5 kwa wakazi zaidi ya 3,000 walioathirika na mradi huo katika wilaya za Mvomero, Kilosa, Mpwapwa na Chamwino.

"Hakuna atakayedhulumiwa, wote mtalipwa fedha zenu kama kawaida," alisema Mang'wela.



Mwenyekiti wa Chama cha Michezo cha Viziwi Mkoa wa Dodoma (DODSA), Japhaly Gama, akigawa vitakasa mikono (sanitizer) kwa washiriki wenye ulemavu wasiosikia kwenye mafunzo ya jinsi ya kuepukana na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona, yaliyotolewa na wataalamu wa afya kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, jijini Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Wafanyabiashara wamwita Jafo sokoni

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAFANYABIASHARA wa matunda na mboga katika soko la Bonanza jijini Dodoma, wamemuomba Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, kulitembelea soko hilo ili kuzibaini changamoto wanazokabiliana nazo.

Wakizungumza na waandishi wa habari wafanyabiashara hao sokoni hapo walisema kuwa hivi sasa viongozi wa jiji wamewatelekeza hali ambayo inasababisha soko hilo kukosa huduma muhimu. Akizungumza kwa niaba ya wafanyabiashara wenzake, Daniel Mvanga, alisema soko hilo limetelekezwa na jiji hali ambayo inasababisha hata taka zinazozalishwa katika eneo hilo kutelekezwa zaidi ya mwezi mmoja bila kuondolewa. Alisema taka hizo ambazo zimetelekezwa kwa zaidi ya mwezi mmoja sasa zimekuwa kero kwao kutokana na kuhatarisha afya zao pamoja na watumiaji wengine wa soko hilo.

Mvanga, alisema kuwa kutokana na taka hizo kukaa kwa zaidi ya mwezi katika eneo la soko hilo wamelazimika kuchangishana kiasi cha Sh. milioni tatu ili kukodi malori pamoja na kijiko kwa ajili ya kuzoa na kuzipeleka dampo la Chidaya nje kidogo ya Jiji la Dodoma.

"Tunamuomba Waziri Jafo aje hapa kwani toka serikali imehamia hapa hakuna kiongozi hata mmoja amekuja kulitembelea soko hili ndio maana tunaonekana kutengwa na kutelekezwa bila kupata msaada wowote kutoka kwa jiji," alisema Mvanga.

Naye mfanyabiashara Dauda Abdul, alisema kuwa ili kuziondoa taka hizo wamelazimika kuchangishana kiasi cha Sh. 80,000 kwa kila mmoja wao ili kuziondoa taka hizo.

Alisema kiasi hicho walichokitoa kila mfanyabiashara ni kikubwa hasa ukizingatia hivi sasa biashara zimekuwa mbaya kutokana na uwepo wa mlipuko wa ugonjwa wa corona.

Vilevile, alisema jiji wamewaletea samansi ya mahakani ikiwata kutoa taka hizo hali ambayo inawashangaza kwani jukumu hilo lipo chini yao.

"Tunaomba kama inawezekana sisi tuendelee kulipa ushuru hata kama tunavyo vitambulisho vya wajasiriamali kwani mzigo huu wa milioni tatu kwajili ya kuondoa taka hizi hatuuwezi, jiji wanadai tusilete hizi taka, lakini kwetu kubeba ndizi bila kuwa na haya majani ni sawa na mtu mzima atembee bila kuvaa nguo," alisema. Akitolea ufafanuzi wa jambo hilo, Ofisa Masoko wa Jiji la Dodoma, James Yuna, alisema wafanyabiashara hao wanatakiwa kuziondoa taka hizo kwani ni zile ambazo zimezalishwa kutoka kule ziliko toka bidhaa zao.

"Hizi taka ni zile ambazo zimekuja kama vifungashio hivyo basi sheria inasema kuwa mtu akiingiza bidhaa zenye taka ambazo hazijazalishwa ndani ya soko wajibu wa kuzitoa ni juu yake," alisema Yuna.

# Hospitali yaambiwa ijiandae kwa corona

**Na Paul Mabeja,** CHAMWINO

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Selemani Jafo, ameutaka uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino mkoani Dodoma, kukamilisha mahitaji muhimu ya Hospitali ya Wilaya hiyo.

Hispitali hiyo iko katika hatua za ukamilishaji wa ujenzi kwa tahadhari ya kupokea wagonjwa wa corona endapo hali ya maambukizi itaendelea nchini.

Jafo aliyasema hayo alipotembelea Hospitali hiyo inayojengwa katika eneo la Mlowa Wilayani Chamwino na kukuta ujenzi katika hatua za ukamilishaji kisha kutoa rai hiyo kwa viongozi kujiandaa mapema na janga hilo la kidunia.

Alisema kutokana na jiografia ya hospitali hiyo kuwa imejitenga na maeneo ya makazi ya watu anashauri waandae jengo moja maalumu na walikamilishe ili endapo janga hili likiendelea, jengo hilo litumike kwa ajili ya kutoa huduma kwa wagonjwa wa corona.

"Kwa hali tuliyonayo sasa hatutakiwi kukaa kusubiria mpaka hali iwe mbaya zaidi tunatakiwa kuendelea kujikinga na kuchukua tahadhari za awali kabisa ikiwa ni pamoja na kuandaa maeneo ya kutolea huduma kwa ajili ya kukabiliana na ugonjwa huu hatari, na hospitail yetu hii naona inafaa kabisa kwa kuwa ina sifa zote," alisisitiza Jafo.

Wakati huo huo, Waziri Jafo aliwapongeza viongozi wa Halmashauri ya Chamwino kwa kusimamia kwa makini ujenzi wa Hospitali hiyo na kuhakikisha kuwa inakamilika kwa ubora wa hali ya juu na kwa wakati.

"Nimefurahi kukuta ujenzi umefikia katika hatua hii ya ukamilishaji, vitu vidogo sana ndio vimebakia kumalizia kabisa ujenzi na majengo yote yanaonekana kuwa na ubora wa hali ya juu hakika nimefurahishwa na hatua hii na hongereni sana," alisema Jafo.

"Haya kwangu mimi naona kama ni mafanikio kwani mwanzoni hali ilikuwa mbaya, ujenzi ulikuwa unasuasua... nilitumia nguvu kufuatilia na kusimamia, lakini kwa sasa wote tunajivunia mafanikio haya huu ndio uongozi wa pamoja unaotakiwa katika utekelezaji wa miradi," alisema Jafo.

Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino ni miongoni mwa Hospitali za Halmashauri 71 zinazoendelea kujengwa nchini kote kupitia mpango wa maboresho wa huduma za afya unaosimamiwa na Ofisi ya Rais (Tamisemi).





## Tulia Trust yasaidia chama cha bodaboda

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TAASISI ya Tulia Trust inayomilikiwa na Naibu Spika, Dk. Tulia Akson, imekidhamini Chama cha waendesha pikipiki za abiria (Bodaboda) cha Jiji la Mbeya, mkopo wa pikipiki saba, kwa lengo la kukiongezea mtaji.

Mkopo huo ulikabidhiwa juzi kwa viongozi wa chama hicho na Meneja wa Taasisi hiyo, Jacqueline Boaz, ambapo alisema taasisi hiyo inalenga kuwasaidia vijana hao kumiliki vyombo vyao wenyewe badala ya kuendesha pikipiki za watu wengine.

Alisema mkopo huo umetolewa na Kampuni inayouza pikipiki hizo ya TVS, na kwamba Tulia Trust inabaki kuwa mdhamini na vijana hao watatakiwa kulipa kidogo kidogo mpaka watakapomaliza kulipa.

"Pikipiki hizi zina thamani ya Sh. milioni 24, pesa hizi zinaonekana kuwa nyingi sana, lakini kwa umoja wenu mhakikishe mnaulipa kwa wakati ili na wengine wapate, na mkilipa kwa wakati mtakuwa na nafasi ya kukopesheka tena," alisema Boaz.

Alisema Taasisi yake itaendelea kufuatilia mwenendo wa urejeshaji wa mkopo huo mpaka mwisho ili kuhakikisha vijana hao wanalipa kwa wakati.

Akipokea kwa niaba ya wanachama wa chama cha bodaboda Jiji la Mbeya, Mwenyekiti wa chama hicho, Aliko Funda, aliishukuru taasisi ya Tulia Trust kwa kuwasaidia kupata pikipiki hizo kwa masharti nafuu ikiwamo kulipa kidogokidogo.

Alisema yeye kama kiongozi wa chama hicho atashirikiana na wenzake kuhakikisha mkopo huo unarejeshwa haraka ili wakope zingine mpaka kila mwanachama awe na pikipiki yake mwenyewe.

"Sisi hatupendi kuendesha pikipiki za wengine, lakini kutokana na mazingira kuwa magumu ndio maana huwa tunalazimika kufanya hivyo, mkopo huu ni mwanzo wa sisi kumiliki vyombo vyetu wenyewe," alisema Funda.

Alisema mkopo huo umewaongezea nguvu kwa maelezo kuwa kuna mkopo mwingine huwa wanapata kutoka katika Halmashauri hiyo unaotokana na asilimia 10 ya mapato ya ndani ambayo huwa inatengwa kwa ajili ya vikundi vya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu.

Mmoja wa waendesha pikipiki hizo, Aman Kidakule, alisema pikipiki za matajiri ambazo wamekuwa wakiendesha zinawatesa kwa sababu wanawekewa malengo makubwa na hivyo kuwafanya washindwe kufanya maendeleo.

Alisema baadhi ya matajiri huwa wanawataka kupeleka Sh. 10,000 kama malengo kwa siku pesa ambazo alisema ni vigumu kupata kipindi hiki ambacho pikipiki ziko nyingi.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa waendesha pikipiki za magurudumu matatu (Bajaji) Jiji la Mbeya, Idd Ramadhan, ambaye pia alihudhuria kwenye makabidhiano ya mkopo huo, aliishukuru taasisi ya Tulia Trust kwa kuendelea kuwadhamini vijana.

Alisema hivi karibuni taasisi hiyo ilidhamini mkopo wa bajaji kwa chama chake, na kwamba wanaendelea kurejesha mkopo huo kupitia benki, na kwamba ndani ya muda mfupi watamaliza kurejesha mkopo huo.

Aliwataka wenzao wa bodaboda kuwa waaminifu kwenye urejeshaji wa mkopo huo ili wamalize haraka na wawe na uwezo wa kukopesheka tena.

# Rufani Mbeya sasa mwendo wa barakoa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

UONGOZI wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mbeya, umetangaza kuwa kila mwananchi anayeingia ndani ya eneo la hospitali hiyo kupata huduma ama kuona wagonjwa lazima awe amevaa barakoa ili kuepuka kusambaa kwa virusi vya corona.

Taarifa ya masharti hayo ilitolewa juzi kwa vyombo vya habari na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano wa Hospitali hiyo, Agrey Layson, ambaye alisema lengo la utaratibu huo ulianza kutekelezwa Aprili 23, mwaka huu. Layson alisema mbali na kuvaa barakoa hizo, pia hospitali hiyo imeandaa utaratibu wa kumpima joto la mwili kila mwananchi atakayekuwa anaingia hospitalini hapo ili kubaini kama hana viashiria vya ugonjwa huo.

"Hatua hii ni sehemu ya mkakati wa taasisi wa kuhakikisha wagonjwa, ndugu wa wagonjwa, wafanyakazi wa hospitali pamoja na wadau wetu wanakuwa salama dhidi ya maambukizi ya virusi vya corona," alisema Layson.

Vilevile, alisema kila mwananchi anatakiwa kusafisha mikono kwa kutumia vitakasa mikono kila anapoingia na kutoka ndani ya eneo la hospitali hiyo ili kuendelea kuwakinga wao wenyewe pamoja na wengine wanaochangamana nao.

Alisema wameandaa utaratibu maalum wa kutoa elimu kwa wananchi ili kuhakikisha kila mmoja anaitikia wito wa kuvaa barakoa na kutakasa mikono bila kulazimishwa kwa maelezo kuwa kuna baadhi bado elimu inaweza ikawa haijawafikia.

Pia, alisema kila mwananchi wa Mkoa wa Mbeya anatakiwa kuhakikisha anaendelea kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa huo kwa maelezo kuwa ni hatari na unakwamisha shughuli mbalimbali za kijamii na kiuchumi.

Alisema elimu na maelekezo ya wataalamu wa afya pamoja na Serikali kuhusu kujikinga na ugonjwa huo ikizingatiwa na kila Mtanzania vita dhidi ya ugonjwa huo itafanikiwa na utatokomezwa haraka.

Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mbeya imekuwa ni miongoni mwa taasisi za afya nchini ambazo zimetoa masharti ya watu wanaoingia katika eneo lake kuvaa barakoa.



Baadhi ya vijana wakipakia ng'ombe kwenye lori katika eneo la Joshoni wilayani Mbeya juzi, kwa ajili ya kusafirishwa kwenda jijini Dar es Salaam kibiashara. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Polisi yatahadharisha madereva, makondakta

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

JESHI la Polisi mkoani Mbeya limewatahadharisha madereva na makondakta wa magari ya abiria mkoani humo, ambao hawatekelezi maagizo ya Serikali kuhusu kukabiliana na maambukizi ya virusi vya corona.

Akizungumza na baadhi ya wajasiriamali wa Soko la Kiwira wilayani Rungwe, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Ulrich Matei, alisema baadhi ya magari bado yanaendelea kujaza abiria kupita kiasi licha ya serikali kuzuia.

Alisema katika uchunguzi wake alibaini kuwa magari yanayoongoza kwa kukiuka utaratibu huo ni yale yanayofanya safari zake kati ya Jiji la Mbeya na Wilaya ya Kyela, ambayo alisema bado yanazidisha abiria kiasi kwamba wengine wanasimama.

Kamanda Matei alimwagiza Mkuu wa Polisi wa Wilaya ya Rungwe kuanza oparesheni maalumu ya kukagua magari hayo na kuwashughulikia madereva na makondakta watakaobainika kujaza abiria kupita kiasi.

Vilevile alisema baadhi ya magari hayo hayana maji na sabuni kwa ajili ya abiria kunawa na hivyo akawatahadharisha wahusika kuwa atakayepatikana atashughulikiwa kwa mujibu wa sheria.

"Nimebaini kuwa kuna watu bado wanafanya mzaha, sasa tunaanza oparesheni zetu za kufanya ukaguzi kwenye magari yote ya abiria na atakayebainika lazima ashughulikiwe na awe mfano kwa wengine, Serikali inapambana na elimu inatolewa kila siku lakini kuna watu bila nguvu hawawezi kuelewa," alisema Kamanda Matei.

Aidha, aliwataka madereva wa magari makubwa (malori) kuhakikisha wanakuwa na vitakasa mikono kwenye magari yao na kuvitumia ili kuepuka maambukizi ya ugonjwa huo.

Vilevile Kamanda Matei alisema Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na vyombo mbalimbali vya dola vinaendelea kulinda mpaka wa Tanzania na Malawi wa Kasumulu wilayani Kyela ili kuwadhibiti watu wote wanaoingia nchini kupitia njia za panya.

Alisema mtu yeyote anayeingia nchini ni lazima afuate taratibu kwa kupitia katika mpaka halali na kwamba yeyote atakayekamatwa akiingia kupitia njia zisizorasmi atashughulikiwa kwa mujibu wa sheria.



# Soko la jioni Darajani kusitishwa

**Na Hawa Abdallah,**
ZANZIBAR

MKOA wa Mjini Magharibi umeuagiza uongozi wa Baraza la Manispaa ya Mjini kusitisha shughuli za soko la jioni katika soko kuu la Darajani ili kupunguza mkusanyiko wa watu.

Mkuu wa Mkoa huo, Hassan Khatib Hassn, ndite aliyetoa agizo hilo katika mkutano maalum na uongozi wa Baraza hilo katika ofisi za Manispaa hiyo, Malindi Mjini Unguja.

Alisema ili kuendeleza shughuli za wafanyabiashara hao, kwa sasa wahamishiwe Amani katika eneo la kiwanja cha ofisi ya mkuu wa mkoa huo kwa muda hadi hali ya maambukizi maradhi ya covid -19 itakapopungua.

Aidha, aliutaka uongozi wa Manispaa hiyo kusitisha mikataba ya askari wanaosimamia shughuli za masoko ndani ya manispaa hiyo kwa kukosa ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yao, jambo ambalo limekuwa likirudisha nyuma maendeleo ya manispaa ikiwamo usimamizi wa masoko hayo sambamba na kupelekea upotevu wa mapato ya serikali. Aliwasisitiza watendaji wa manispaa hiyo kutoa matangazo maalum na maagizo kwa wafanyabiashara wakiwamo wa maduka na taasisi zinazotoa huduma kwenye manispaa hiyo kuweka ndoo na dawa za kunawia mikono kabla ya kutoa huduma.

Alisema wakati Taifa likipambana na maradhi hayo mtu yeyote katika mkoa huo akibainika kwenda kinyume cha maagizo na maelekezo ya serikali kupitia wataalamu wa afya juu ya tahadhari, atachukuliwa hatua ikiwamo kutozwa faini na kufungiwa biashara yake.

Mapema Mkurugenzi wa Manispaa ya Mjini, Said Juma Ahmada, alisema uongozi ulishatoa mapendekezo ya kuhamisha wa soko la jioni kwa muda na ameahidi kuyafanyia kazi maagizo na maelekezo hayo kwa haraka.

Kabla ya mkutano huo Mkuu wa Mkoa alifanya ziara katika maeneo mbalimbali ya utoaji huduma katika mkoa huo ikiwamo soko la Mwanakwerekwe na Bandari ya Malindi Mjini Unguja.



Mwendesha baiskeli, akiikokota huku ikiwa imesheheni magunia ya mkaa wakati akipanda mlima katika eneo la Mvuti Chanika, nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam, jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Polisi lawamani kukwama kesi udhalilishaji kijinsia

**Na Hawa Abdallah,**
ZANZIBAR

BAADHI ya vituo vya Polisi vimelalamikiwa kwamba vinafanya uzembe na kuchukua muda mrefu wa kufuatilia upelelezi wa kesi za udhalilishaji zinazoripotiwa.

Hali hiyo imesababisha wananchi kukosa imani na utendaji kazi wa vituo hivyo.

Wakizungumza na mwandishi wa habari hizi, baadhi ya waathirika waliofanyiwa vitendo vya udhalilishaji wa watoto wao kwa nyakati tofauti katika Mkoa wa Kusini Unguja katika vijiji vya Hanyegwa Mchana, Kizimkazi na Jambiani.

Walisema muda mrefu kesi zao zipo vituoni, lakini wanapewa majibu kesi hizo zinafuatiliwa, majibu ambayo hayaridhishi na hayatoi matumaini ya haki kupatikana.

Walisema wamekuwa wakienda Polisi kufatilia kesi za watoto wao ambao matokeo yao yametokea kwa vipindi tofauti, lakini wanakosa kupata majibu mazuri jambo ambalo linaonyesha uwajibikaji kwa baadhi ya polisi ni wa kusuasua.

Mama wa mtoto aliyefanyiwa shambulio la aibu huko Jambiani, alisema ni mwezi wanne sasa hajapata jibu la uhakika kuhusu suala la mwanawe, zaidi na kituo kudai mshtakiwa hajapatikana wakati anaonekana akirandaranda mitaani.

Alisema amekosa imani na Jeshi hilo kutokana na kuona kuwa hasaidiwi kupata haki.

"Mimi kwa sasa sina imani na yoyote kwani naamini hakuna haki itakayotendeka ni bora tu nikae kwani Mungu anatosha," alisema.

Mama wa mtoto ambae alilawitiwa huko Hanyegwa Mchana na kesi yake kuripoti kituo Cha Polisi Chwaka, alisema amekuwa na kawaida ya kufatilia, lakini mara ya mwisho jibu ambalo alipewa ni kuwa mtuhumiwa ni mtoto wa miaka 13, hivyo hawezi kushtakiwa kwa mujibu wa sheria.

Alisema jibu hilo halikumridhisha kwa kuwa taarifa alizonazo ni kuwa mtuhumiwa ana umri wa miaka 15.

Tukio hilo lilitendeka Novemba mwaka jana na mtoto huyo aliumia vibaya na kulazwa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa siku tatu.

Mkuu wa Upelelezi wa Jeshi hilo Mkoa wa Kusini Unguja, Ramadhan Khamis, alisema matukio yote wameyafutilia.

Kuhusu la Jambiani, alisema Polisi inaendelea kumtafuta mshtakiwa na atakapopatikana atachukuliwa hatua.

Kuhusu tukio la Hanyegwa Mchana, alisema jalada la kesi hiyo lilipelekwa Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) na lilirejeshwa huku wakitakiwa jalada hilo lifungwe kwa kuwa mtuhumiwa kutokana na umri, hawezi kishtakiwa.

Mratibu wa Wanawake na Watoto kutoka Cheju, Hidaya Ali Rajab, alisema mshtakiwa ni mtoto wa miaka 15 na sio 13 na kinachofanyika hapo ni dhahiri kuwa kuna udanganyifu umefanyika.

Nae Naibu Sheha wa Jambiani, Kijigija Upatu Haji, alisema inaonekana kuwapo harufu ya rushwa vituoni kutokana na matukio hayo kuchukua muda mrefu kupatiwa ufumbuzi.

Alisema kwa mfano tukio la hivi karibuni katika shehiya hiyo kuwa mtuhumiwa hajakamatwa, huku akionekana mitaani.

Hivyo alisema kuwa kuendelea kuwapo kwa hali hiyo, kunapelekea kuongezeka kwa matukio hayo kwa kuwa watuhumiwa wataona hakuna wanachofanywa.

Alisema kwa mwaka 2021 ndani ya shehiya yake yametokea matukio matatu, ambapo moja linamhusu mtoto wa miaka mitano aliebakwa mara mbili na watu wawili tofauti. Alisema na shauri lingine lipo mahakama ya watoto Vuga na lingine linafanyiwa utaratibu wa kufikishwa mahakamani.

Tukio moja ni la shambulio la aibu ambapo mtuhumiwa hajapatikana.

# Waishukuru SMZ ujenzi wa mitaro

**Na Hawa Abdallah,**
ZANZIBAR

BAADHI ya wananchi wanaoishi katika maeneo ambayo awali yalizoeleka kujaa maji katika kipindi cha mvua za masika, wameishukuru serikali kwa jitihada za kuondosha kadhia ya kuingiliwa na maji.

Wametoa shukrani kwa serikali kutokana na ujenzi wa mitaro ya kupitishia maji.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti walisema, ujenzi wa mitaro hiyo umesaidia kwa kiasi kikubwa kuondokana na hali ya nyumba zao kutuama maji katika kipindi hiki cha mvua mkubwa zinazoendelea kunyesha katika maeneo mbalimbali.

Mjumbe wa Sheha wa Shehia ya Mpendae kwa Bitihamran, Ayoub Mohammed, alisema mtaro huo kwa kiasi kikubwa umewasaidia kuondokana na kadhia ya kuhama makazi yao katika kipindi hichi cha mvua kutokana na makazi yao kujaa maji.

Alisema kabla ya ujenzi wa mtaro huo katika kipindi hiki cha mvua wakazi wa maeneo hayo walilazimika kuhama ili kunusuru maisha yao kutokana na maeneo hayo kufurika maji mengi, hali iliyokuwa ikiwaletea athari kubwa.

"Hapo awali kabla ya ujenzi huu wa mtaro tulilazimika kuhama makazi yetu kwa kipindi cha miezi mitatu hadi pale maji yatakapokauka kabisa ndio tunarudi katika majumba yetu... lakini sasa tunashukuru maji hayaingii katika makazi yetu, kwa hilo tunaendelea kuipongeza serikali kwa kila jitihada wanazochukua katika kuwajali wananchi wake," alisema.

Nae, Tatu Khamis Said, mkazi wa maeneo hayo, alisema katika kulinda mtaro huo wameweka utaratibu maalum wa kuusafisha mara kwa mara kwa kutoa majani na taka ili kuepusha maji kutuama na kuona yanakwenda kama kawaida.

Mratibu wa Mradi wa Huduma za Jamii Mijini (ZUSP) kutoka Wizara ya Fedha na Mipango, Makame Ali Makame, aliwaomba wananchi kuhakikisha wanakuwa walinzi kwa kuacha tabia ya kutupa taka jambo ambalo linaweza kuleta athari ikiwamo mafuriko.

## MATANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676

### KUPOTEA KWA CHETI



115713102

**GLORY L. LOSARU** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.1818-0036** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **BARAA SEKONDARI** mwaka 2009. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **KJN/RB/8074/2016.**

### KUPOTEA KWA VYETI



115713002

**PAUL MAKUNGU MBOJE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S3853/0061** kilichotolewa na NYARUGUSU SEKONDARI mwaka 2011. Cheti cha kidato cha sita chenye index namba S0155/0552 kilichotolewa na TABORA BOYS HIGH SCHOOL mwaka 2014. Cheti cha kuzaliwa chenye namba **C/NO.02195995.** Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **MAG/CID/BI/I/VOL.XXII/32.**

**UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA AT BUKOBA**

**LAND CASE NO. 7/2017**

**PATRICK MWOMBEKI ......................................PLAINTIFF**

**VERSUS**

**WILBARD MWOMBEKI AND ANOTHER ..............DEFENDANTS**

**TO, ANTIDIUS KAMUGISHA**

**RE: NOTICE OF DATE OF MEDIATION**

Whereas the above mentioned Applicant has lodged a case registered as Land Case No. 7 of 2017 against you at the High Court of Tanzania at Bukoba.

Take notice that the above said case has been scheduled for mediation on 29th day of April, 2020 at 09:00 am before Hon. Judge F. H.Mtulya. You are authorized to appear in person or through your Advocate.

Take further notice that in default of your appearance on that date and time for the said mention the case will proceed in your absence.

Given under my hand and seal of the court this 16th day of April, 2020.




**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika mahakama ya mwanzo:**
**CHAMWINO-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;18/2020**

**Ombi la MOHAMED O.MOHAMED**
**Kuteuliwa msimamizi wa mirathi**
**marehemu ASHA ALLY**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 28/04/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 23/04/2020.



**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati ya mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KITAIFA




Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Anna Mghwira (katikati), akipokea lita 2,500 za vitakasa mikono kutoka kwa Meneja Mkuu wa Kampuni ya Mega Beverages,Chris Ndosi (kulia) vilivyotolewa na kampuni hiyo kwa ajili ya kupambana na Corona katika hafla iliyofanyika mjini Moshi, jana. Kushoto ni Katibu Tawala wa mkoa huo, Dk. Hatibu Kazungu. **PICHA: MPIGAPICHA** WETU.

# Msalaba Mwekundu yasaidia waathirika mafuriko

**Na Restuta Damian,** MISSENYI

KAIMU Mkuu wa Wilaya Missenyi mkoani Kagera, Godfrey Mheruka, amewataka waathirika wa mafuriko katika kijiji cha Bunazi na Mutondo, waliopo kambini baada ya nyumba zao kujaa maji kujikinga na maambukizi ya ugonjwa wa Covid-19.

Alitoa tahadhari hiyo baada ya kupokea vifaa vya msaada wa magodoro, ndoo, madumu, vyandarua, blanketi na mikeka kutoka Shirika la Msalaba Mwekundu kwa waathirika 41 waliopo kwenye kambi hiyo.

Mheruka alisema, licha ya changamoto ya makazi kusombwa na maji, jamii lazima iendelee kuzingatia hatua za kujilinda na maambukizo.

"Hii itafanya wilaya, mkoa na taifa kuwa salama zaidi, mafuriko yasipoteze kumbukumbu ya kuchukua tahadhari ya mapambano ya ugonjwa huo hatari, wananchi zingatieni," alitahadharisha.

Mratibu wa maafa wilayani hapo, Raphael Maigize, alisema katika kijiji cha Mutondo kaya 32 zimeathiriwa na mafuriko hayo. Pia kijiji cha Bunazi kaya 21 zilipelekwa kambini.

Naye Mwenyekiti wa Shirika la Msalaba Mwekundu wilayani humo, Leonard Kachebonaho, alisema Shirika hilo limetoa vifaa hivyo ili kuwalinda watoto wasipate magonjwa yatokanayo na baridi.

"Nimetoa ndoo 100, madumu ya maji 56, magodoro mawili, mikeka 56, blanketi 56, vyandarua 150 ikiwa ni sawa na huduma ya kwanza kwa mtu aliyepatwa na maafa," alisema.

# Abiria ATCL lazima barakoa

**Na Romana Mallya**

KAMPUNI ya Ndege ya Tanzania (ATCL) imewataka abiria wake wanaosafiri na ndege zao, kuhakikisha wanavaa barakoa kabla na wakati wote wa safari.

Kwa mujibu wa taarifa ya kampuni hiyo iliyotolewa jana na Mkurugenzi Mtendaji, Mhandisi Ladislaus Matindi, uongozi wa ATCL unawataka abiria kuvaa barakoa pamoja na wale wanaofika kwenye ofisi zao na kwamba kinyume cha hivyo, hawatahudumiwa.

"Abiria na wateja wetu hawatahudumiwa katika vituo na ofisi zetu mahali popote bila ya kuvaa barakoa," alisema.

Matindi alisema ATCL inaendelea kuchukua tahadhari zote za kiusalama kuhakikisha afya za wafanyakazi, abiria na wateja kwa ujumla zinalindwa kama inavyoelezwa na Wizara ya Afya.

"Tunaendelea kutoa huduma katika safari za ndani vituo vyote 11 ambavyo ni Dar es Salaam, Zanzibar, Kilimanjaro, Mwanza, Bukoba, Kigoma, Tabora, Dodoma, Mpanda, Iringa na Mbeya," alisema.

Matindi alisema wameanzisha safari za kwenda na kurudi kati ya Kilimanjaro na Mwanza.

# Waziri awabana watendaji fedha za uwekezaji kilimo

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

IDARA ya Sera na Mipango ya Wizara ya Kilimo, imetakiwa kubainisha kiasi cha fedha kilichowekezwa kwenye kilimo kutoka serikalini, sekta binafsi na washirika wa maendeleo.

Agizo hilo lilitolewa jana na Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, alipozungumza na watumishi wa idara hiyo kwenye Ukumbi wa Wizara hiyo, maarufu KILIMO IV jijini Dodoma.

Alisema pamoja na majukumu muhimu yanayofanywa na Wizara ya Kilimo, idara hiyo inapaswa kuongeza juhudi na weledi katika utendaji kazi wake wa kila siku ili kuongeza tija na uzalishaji wa mazao ya wakulima.

Waziri Hasunga aliitaka idara hiyo kubainisha takwimu za uzalishaji wa mazao, bei za mazao na uchambuzi, ikiwa ni pamoja na takwimu za mazao ya mboga, maua na matunda.

Alisema pamoja na mafanikio makubwa ambayo yameonekana katika sekta ya kilimo katika kipindi cha miaka minne ya serikali ya awamu ya tano, bado sekta ya kilimo inapaswa kuimarishwa zaidi ili kuwa na mafanikio makubwa zaidi. "Nchi zilizoendelea duniani zimefanya nini na kwanini Tanzania tupo nyuma kwenye kilimo? Kuna viwanda vingapi vya kuchakata mazao ya kilimo?" Hasunga alihoji wakati wa kikao kazi hicho.

Katika hatua nyingine, Hasunga ameitaka idara hiyo kubainisha kuhusu uongezaji thamani na sera inasema nini kuhusu uongezaji thamani wa mazao.

Aliitaka idara hiyo kubainisha sera ya masoko na wataalamu wanasemaje kuhusu hali ya masoko. Pia akaitaka kufahamu hali ikoje kupitia sera ya usalama wa chakula, Sera ya Ushirika, Sera ya Matumizi Bora ya Ardhi na vikwazo vyake kwenye kilimo.

# Braithwaite aweka matumaini Barca




**BARCELONA, HISPANIA**

MARTIN Braithwaite ana matumaini ya kubakia kwa muda mrefu pale Barcelona wakati kukiwa na uvumi kwamba klabu hiyo ya LaLiga tayari wanaangalia uwezekano wa kumuuza mshambuliaji huyo.

Braithwaite mwenye umri wa miaka 28, aliwasili pale Barca akitokea Leganes Februari katika uhamisho wa 'utata' uliogharimu euro milioni 18, kwa kile kilichoitwa usajili wa dharura.

Wakati ripoti za hivi karibuni zikibainisha kwamba Barcelona wanaweza tayari kufikiria kumuuza Braithwaite, mchezaji huyo wa kimataifa wa Denmark – ambaye alisaini mkataba utakaomuweka hapo hadi mwaka 2024 , bado anafikiria anaweza kubakia hapo kwenye dimba la Camp Nou.

"Nina uhakika nitabakia hapa zaidi ya miaka minne na nusu. Hicho ndicho ninachokiona kichwani mwangu," alisema Braithwaite akiiambia ESPN.

"Kwa sasa, nataka tu kwenda kucheza na kufurahia na kushinda mataji na timu hii kwa sababu ndio maana nipo hapa."

Braithwaite ameichezea mechi tatu Barcelona kabla ya msimu kusimamishwa kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Mshambuliaji huyo wa zamani wa Middlesbrough amejipangia malengo yeye mwenyewe na miamba hao wa Hispania, ambao walikuwa kileleni mwa msimamo wa LaLiga wakati ligi hiyo ilipposimamishwa.

# Bale: Mimi bado shabiki wa Spurs



**MADRID,** Hispania

NYOTA wa Real Madrid, Gareth Bale, anajitambua yeye mwenyewe kama shabiki wa Tottenham na aliumizwa na kufungwa kwao kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya Juni mwaka jana.

Mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Wales, Bale, aliondoka Spurs kwenda kwenye dimba la Santiago Barnabeu kwa ada iliyoripotiwa kuwa pauni milioni 86, Septemba mwaka 2013 na ameshinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya mara nne, huku pia akibeba LaLiga na Kombe la Mfalme [Copa del Rey].

Bale amekuwa hana uhusiano mzuri na kocha wake, Zinedine Zidane, na mara kwa mara akihusishwa na mpango wa kuondoka, huku uhamisho wake wa kwenda kwenye klabu ya Ligi Kuu ya nchini China, Jiangsu Suning ukishindikana Julai mwaka jana.

Pia alifikiriwa kama angerudi Tottenham na Bale amefafanua bado ana mapenzi na klabu hiyo aliyoichezea kati ya mwaka 2007 na 2013, akielezea uchungu wake wa kufungwa na Liverpool kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa mwaka jana.

"Kila mmoja anapenda kuangalia fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, na Tottenham walikuwa pale hivyo nilikuwa na hisia za hali ya juu, nilikuwa natumaini wamefika fainali na watafanya kile walichokusudia," alisema Bale akiiambia BT Sport.

"Walikuwa na mechi nzuri, hasa kwenye nusu fainali dhidi ya Ajax.

"Kwa upande wetu mashabiki wa Tottenham ilikuwa fainali iliyotuumiza, lakini unatakiwa kuangalia picha kubwa. Walifanya kazi kubwa kwa pale walipofikia."

# Klopp awaonya wapinzani EPL




**LIVERPOOL,** England

JURGEN Klopp ametuma salamu kwa wapinzani wao kwa kusisitiza Liverpool "hawajamaliza kurasa" na bado wanaweza kuwa bora.

'Wekundu' hao walikuwa wanaongoza kwa pointi 25 kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu ya England dhidi ya Manchester City, wakiwa wamecheza mchezo mmoja zaidi, wakati msimu ulipositimamishwa kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Msimu wa 2019-20 unaweza kumalizika, halafu Liverpool wanaonekana kwenye nafasi ya kulitwaa taji lao la kwanza la Ligi Kuu kwa kipindi cha miaka 30 na kuongeza mafanikio chini ya kocha, Klopp.

Baada ya kupoteza kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa msimu wa 2017-18, walibeba taji hilo kwa mara ya sita kutokana na kuifunga Tottenham kwenye fainali mjini Madrid, kabla ya kushinda Uefa Super na Klabu Bingwa ya Dunia mwaka 2019.

Hata hivyo, Klopp amesisitiza kuna nafasi ya kuimarika zaidi kwa timu hiyo ambayo imefungwa mara mbili tu kwenye ligi tangu kuanza mwaka uliopita.

Kocha huyo wa Liverpool ameiambia Sky Sports: "Hatutabadilika, hicho ndio kitu cha kwanza, lakini kama tutakuwa bora itategemea na nini klabu nyingine zinafanya kwa sababu zote zina nafasi ya kuimarisha vitu, na kufanya vitu kwa ubora zaidi.

"Hivyo, sina shaka kuhusu majaliwa ya baadaye kwamba sisi tutaendelea kuwa bora. Lakini hatutabadilika. Timu hii haijamaliza kurasa, na tuna nafasi kubwa ya kuimarika na kufanya kazi vizuri.

"Tuna damu changa ndani yetu. Tunaweza kuimarika zaidi na timu hii na kupata mafanikio makubwa."

Klopp, ambaye alichukua nafasi ya kuinoa Liverpool Oktoba mwaka 2015, alikumbana na wakati mgumu pale kwenye dimba la Anfield kabla ya kubeba taji lake la kwanza msimu uliopita.

Liverpool walipoteza kwenye fainali ya Kombe la EFL na Ligi ya Europa msimu wa 2015-16 na walifungwa na Real Madrid kwenye fainali ya ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2018.

## HABARI MICHEZO

# Corona imetibua usajili wa Mbappe - Wakala

**PARIS,** Ufaransa

KYLIAN Mbappe angeuzwa kwa thamani ya euro milioni 300 na alikuwa anakaribia kujiunga na Real Madrid mwaka huu, lakini mlipuko wa virusi vya corona umetibua dili hilo, kwa mujibu wa wakala ambaye amekuwa akifanya kazi mara kwa mara na klabu hiyo ya Ligi Kuu ya Hispania.

Nyota huyo wa Ufaransa, Mbappe mara kwa mara amekuwa akihusishwa na mpango wa kuhamia Santiago Bernabeu licha ya kujiunga na Paris Saint-Germain akitokea Monaco mwaka 2018.

Awali alisaini kwa mkopo, halafu mshambuliaji huyo akasaini mkataba wa kudumu pale Parc des Princes kwa euro milioni 180, na kumfanya kuwa mchezaji wa pili ghali zaidi kwenye historia ya usajili wa klabu hiyo, nyuma ya Neymar aliyesajiliwa kwa euro milioni 222.

'Dogo' huyo mwenye umri wa miaka 21, ametajwa kuwa mmoja wa wachezaji wanaopewa kipaumbele kusajili na Madrid, ingawa PSG imeonyesha nia ya kumbakisha kwa muda mrefu, huku mkataba wake wa sasa ukimalizika mwaka 2022.

Yvan Le Mee, ambaye amekuwa akifanya kazi za usajili na Madrid kwa kufanikisha uhamisho wa Ferland Mendy na Julien Faubert, anafikiri uhamisho wa kwenda kwa miamba hao wenye maskani yao mji mkuu wa Hispania ulikaribia kutimia kabla ya mlipuko wa ugonjwa wa COVID-19 ambao umetibua msimu wote.

Sasa, anaamini dili hilo halitafanyika hadi baada ya mashindano ya Mataifa ya Ulaya, ambayo yamepelekwa hadi mwakani 2021.

"Mbappe, alikuwa tayari kutua Real Madrid, kabla ya kutokea kwa mlipuko wa virusi vya corona uliotibua uchumi wa kila kitu," alisema Le Mee akiliambia gazeti la Marca.



## Qatar yaziomba Klabu EPL zizuie Newcastle kuuzwa

**DOHA,** Qatar

KAMPUNI ya utangazaji ya beIN SPORTS yenye makazi yake nchini Qatar, imeripotiwa kuziomba klabu za Ligi Kuu ya England kuzuia mpango wa kuuzwa kwa Newcastle United.

Newcastle imeripotiwa kwamba inakaribia kuuzwa kwa kampuni ya kigeni kwa fedha nyingi, akihusishwa mfalme wa Saudi Arabia, Mohammed bin Salman, kwa kiasi kinachotajwa kuwa ni pauni milioni 300.

Dili hilo litasimamiwa na Kampuni ya Public Investment Fund ya Saudi Arabia kwa kununua asilimia 80 ya hisa za Newcastle, ambayo imekuwa ikimilikiwa na Mjasiriamali Mike Ashley kwa kipindi cha miaka 13.

Kwa mujibu wa 'umbea' wa habari ulioenea kwenye vyombo vya habari vya Uingereza, beIN SPORTS inazishauri klabu za EPL kupinga ununuzi huo kwa sababu kampuni hiyo ya Saudi Arabia inadaiwa kuhusishwa na mambo ya ukandamizaji wa haki za binadamu na uporaji wa haki za utangazaji.

Kampuni moja ya beoutQ, ambayo inatajwa kuhusishwa na kampuni hiyo imekuwa ikionyesha matukio ya Ligi Kuu ya England kupitia mtandaoni katika miji kadhaa ya nchi za Mashariki ya Kati kwa 'kuiba' haki hiyo.

Katika barua yake, Yousef al-Obaidly, Ofisa Mtendaji Mkuu wa beIN SPORTS, imeripotiwa kwamba imemuambia Mwenyekiti wa Klabu za Ligi Kuu ya England "kuuzwa kwa Newcastle United kutasababisha athari kubwa kwa klabu nyingine na mapato ya kibishara ya Ligi Kuu ya England."

Agosti mwaka 2018, Ligi Kuu ya England iliandika barua ya wazi kuishutumu Kampuni ya beoutQ na kuitangaza beIN kwamba ndio inayoshikilia haki ya matangazo ya Ligi Kuu ya England kwa miji ya nchi za Mashariki ya Kati na miji ya Afrika Kaskazini.

# Vertonghen adokeza kuondoka Tottenham




**LONDON,** England

JAN Vertonghen amesema angependa kujifunza lugha nyingine wakati mlinzi huyo wa Tottenham akidokeza kuhusu kuondoka wakati mkataba wake utakapomalizika mwishoni mwa msimu huu.

Vertonghen mwenye umri wa miaka 32, amekuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka pale Spurs, ambako alitua akitokea Ajax mwaka 2012, na sasa mkataba wake unafikia mwisho.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji hajaondoa uwezekano wa kubakia kwa miamba hao wa Ligi Kuu ya England, lakini amesema Hispania na Italia ndio sehemu mojawapo anayoweza kwenda, huku Inter ikiripotiwa kuhitaji huduma yake.

"Nataka kusajiliwa katika klabu sahihi. Hiyo inaweza kuwa Tottenham, lakini pia klabu nyingine," alisema Vertonghen akiiambia Play Sports Kot Jumatano.

"Kwa vyovyote, inatakiwa kuwa klabu yenye malengo. Na nataka kuendelea kucheza Ulaya kwa sababu timu ya taifa ni muhimu sana kwangu."

Aliongeza: "Ningependa kujifunza lugha nyingine. Kihispania na Kitaliano ni machaguo yangu.

"Muda wa mkataba nitakaopewa ofa ndio utatoa taswira halisi.

## HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# NEYMAR SI KIONGOZI, HAFIKIRII SOKA - RAFAEL

●●● Nasema ukweli, lakini wakati mwingine watu hawataki kuambiwa ukweli...

**PARIS,** Ufaransa

NYOTA wa Paris Saint-Germain, Neymar, si "kiongozi" na anatakiwa kuufanya mchezo wa soka kuwa ndio kipaumbele chake kama anataka kuona mafanikio ya Brazil, kwa mujibu wa beki wa pembeni wa zamani wa Manchester United, Rafael da Silva.

Neymar, mchezaji ghali zaidi duniani baada ya uhamisho wa euro milioni 222 kwenda PSG mwaka 2017, ameendelea kutengeneza vichwa vya habari akihusishwa na uwezekano wa uhamisho wa kurudi kwa mabingwa wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, Barcelona.

Mshambuliaji huyo wa Brazil amekuwa na matukio ya utata nje ya dimba, pia akionekana kumzomea straika wa Borussia Dortmund, Erling Haaland wakati wa mchezo wao wa ushindi wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16-bora.

Rafael, ambaye kwa sasa anacheza kwa wapinzani wa PSG kwenye Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, Lyon, alicheza pamoja na Neymar kwenye kikosi cha timu ya Taifa ya Brazil kwenye michezo ya Olimpiki mwaka 2012 na anaamini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, anaweza kuiongoza Brazil kwenye mafanikio, kama atasikiliza ushauri.

> **Brazil walikuwa wanapewa nafasi kubwa ya kushinda taji la Kombe la Dunia mwaka 2018, lakini walitolewa hatua ya robo fainali kabla ya kutwaa Kombe la Copa America mwaka jana huku Neymar akikosekana kutokana na majeraha ya kifundo cha mguu.**

"Tunamhitaji Neymar, hilo kwa uhakika kabisa," alisema Rafael akiambia ESPN. "Tunamhitaji sana. Anahitaji kuimarika kwenye vitu vingi nje ya uwanja. Ni mwanasoka muhimu.

"Anahitaji kuimarika sana nje ya uwanja na kuingia ndani ya dimba na kufanya vitu kwa ubora wake. Natumaini anaweza kufanya hivyo na kama akifanya tunakuwa na nafasi kubwa ya kushinda.

"Neymar si kiongozi. Sidhani kama ni kiongozi. Si yeye. Anaweza kufanya vitu anavyofanya kwa sababu ni mzuri, kama akiamua kutulia na kujikita kwenye soka, yeye ndiye mchezaji bora duniani."

Rafael aliongeza: "Mpira wa miguu unatakiwa kuwa kipaumbele chake cha kwanza katika maisha. Ana vitu vingi mno vinavyomzunguka. Anafikiria kwenye akili yake 'sitaki kufanya kile' kucheza vizuri, lakini anahitajika kufanya hivyo.

"Namjua na nimcheza ji ninayemjua, ni mtu mgumu mno kusikiliza ushauri. Hili si jambo zuri kwake.

"Nasema ukweli, lakini wakati mwingine watu hawataki kuambiwa ukweli. Wanataka tu uwaambie wewe ni mzuri sana, ni wa maajabu na wanataka uwaambie mazuri tu, lakini maisha hayapo hivyo.

"Nafikiri anahitaji kusikiliza zaidi na kama atafanya hivyo, itakuwa ngumu mno kuizuia Brazil."

## KWA UFUPI

### PSG KUMFUNGA MBAPPE

KLABU ya Paris St-Germain imeamua "kumfunga" mshambuliaji wa Ufaransa, Kylian Mbappe, mwenye umri wa miaka 21, katika mkataba wake mpya kutokana na changamoto ya kushuka thamani yake wakati wa kipindi cha majira ya joto kutokana na mlipuko wa virusi vya corona. (ESPN)

### CHELSEA KUMPOTEZEA CHILWELL

KLABU ya Chelsea inapanga kuachana na mpango wao wa kuwania kumsajili beki wa pembeni wa Leicester na timu ya Taifa ya England, Ben Chilwell mwenye umri wamiaka 23. (Sun)

### BECKHAM KUMSAJILI RODRIGUEZ

MMLIKI wa klabu ya Inter Miami, David Beckham amezungumza na Real Madrid kuhusu uwezekano wa kumsajili mshambuliaji wa kimataifa wa Colombia, James Rodriguez, mwenye umri wa miaka 28. (Goal)

### KIPA LIVER KUTUA WOLVES

GOLIKIPA wa Liverpool, Loris Karius mwenye umri wa miaka 26, anapanga kujiunga na Wolves kwa mkopo msimu ujao. (Fantatikh)

### CAVANI ATAKIWA NEWCASTLE

MMILIKI mpya anayetaka kuinunua Newcastle United ameonyesha nia ya kutaka kumsajili mshambuliaji wa Paris St-Germain na timu ya Taifa ya Uruguay, Edinson Cavani mwenye umri wa miaka 33, huku pia kukiwa na matumaini ya kumchukua kocha mmoja kati ya Massimiliano Allegri au Mauricio Pochettino. (ESPN)

### ARSENAL WAMUWANIA PARTEY

KLABU ya Arsenal imefungua mazungumzo na Atletico Madrid juu ya uwezekano wa kumsajili mchezaji wa kimataifa wa Ghana, Thomas Partey, mwenye umri wa miaka 26, kwa mujibu wa baba mzazi wa kiungo huyo. (Daily Mail)

### SPURS KUMFUATA EMERSON

TOTTENHAM Hotspurs inawania kumsajili beki wa pembeni wa Real Betis raia wa Brazil, Emerson mwenye umri wa miaka 21, ambaye anamilikiwa pia na Barcelona. (Mundo Deportivo)

### CHELSEA, ATLETICO VITANI

CHELSEA ipo kwenye mbio moja na Atletico Madrid kuwania kumsajili mchezaji, Mohamed Sankoh mwenye umri wa miaka 16, anayechezea kikosi cha Uholanzi chini ya umri wa miaka 21 kutokea Stoke. (Goal)

### MKONGOMANI KURUDI EVERTON

WINGA wa kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Yannick Bolasie mwenye umri wa miaka 30, anapanga kurudi Everton baada ya Sporting Lisbon kukatisha muda wake wa kucheza kwa mkopo ili kupunguza gharama. (A Bola)

### SCHALKE KUACHANA NA KENNY

KOCHA wa Schalke, David Wagner, amesema klabu hiyo haitatoa ofa ya kumsajili Jonjoe Kenny mwenye umri wa miaka 23, kutoka Everton kwa mkataba wa kudumu, lakini wangependa kuongeza muda wake wa kucheza kwa mkopo kwa msimu mmoja zaidi. (Sky Sports)

### NEYMAR KUKATWA MSHAHARA

STRAIKA wa Brazil, Neymar, mwenye umri wa miaka 26, atatakiwa kukatwa mshahara wa pauni milioni 26 kama anataka kuhamia Barcelona kutoka Paris St-Germain kipindi kinachokuja cha majira ya joto. (Mundo Deportivo)

HABARI MICHEZO

# CHAMAZI WAIPA JEURI AZAM KUMALIZA YA PILI

**Na Saada Akida**

KUKAMILIKA kwa Uwanja wa Chamazi uliokuwa katika matengenezo, kumeipa matumaini Azam FC ya kumaliza katika nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu Bara wakati ligi hiyo itakaporejea hapo baadaye, imeelezwa.

Ligi Kuu Bara imesimama kwa kipindi kisichojulikana kutokana na kuibuka kwa ugonjwa wa COVID-19, unaosababishwa na virusi vya corona, na hadi inasimama Azam FC ipo nafasi ya pili ikiwa na alama 24 baada ya mechi 28, ikizidiwa alama 27 na Simba iliyopo kileleni huku Yanga iliyoshuka dimbani mara 27 ikiwa na pointi 51 ikifuatiwa na Namungo FC pointi 50.

Mtendaji Mkuu wa Azam, Abdukarim Amin 'Popat' ameliambia gazeti hili kuwa uwanja wao umekamilika kwa asilimia 100, hivyo utaanza kutumika ligi itakaporejea.

Alisema kurejea kutumia uwanja wao wa nyumbani kutawasaidia kufikia malengo yao ya kuhakikisha wanafanya vizuri katika michezo iliyobaki ili kujihakikishia kumaliza msimu wakiwa nafasi ya pili. "Tuna imani ligi itakaporejea tutaendelea kutumia uwanja wetu wa Azam Complex [Chamazi], hii itatusaidia kufanya vizuri katika michezo iliyobaki," alisema Popat.

Alisema kwa mujibu wa kocha wao, Aristica Ciaoba, alitoa malalamiko juu ya kuathirika kwa kikosi chao kutokana na kutumia uwanja wa mazoezi Chamazi ambao ulitengwa kwa ajili ya kufanya mazoezi na kwenda kucheza Taifa au Uhuru.

"Kubadilisha uwanja kulituathiri kidogo, ukiangalia tunafanya mazoezi katika uwanja wetu wa nyasi halisi na kwenda kucheza Uwanja wa Uhuru au Taifa, hii imechangia pia kutofanya vizuri baadhi ya michezo yetu," alisema Popat.

Uwanja huo ulikuwa unafanyiwa ukarabati ambapo nyasi zote zilifumuliwa na kuanza kuwekwa upya kabisa na inaelezwa kuwa zaidi ya bilioni tatu zimetumika kuukarabati.

Wakati wa maboresho Azam FC walikuwa wanatumia Uwanja wa Uhuru na Taifa kwenye mechi zao za nyumbani, ambapo sasa watarejea Chamazi.

SI VITA...



Nahodha wa Yanga, Papy Tshshimbi (kushoto), akiwa na ndugu zake tayari kwa kufanya mazoezi binafsi nyumbani kwa kiungo huyo jijini Dar es Salaam juzi, katika kipindi hiki ambacho klabu yake imesitisha mazoezi ya pamoja kutokana na mlipuko wa maambukizi ya virusi vya corona duniani vinavyosababisha ugonjwa wa COVID-19. **MPIGAPICHA WETU**

# Dulla Mbabe sasa ajifungia

**Na Shufaa Lyimo**

BONDIA wa Ngumi za kulipwa nchini, Abdallah Pazi (Dula Mbabe), amelazimika kubadili programu yake ya mazoezi na kuanza kukimbia asubuhi na jioni kwa lengo la kuweka mwili wake sawa kabla ya kurejea nyumbani na kujifungia akijifua yeye binafsi ili kujiepusha na maambukizo ya virusi vya corona.

Akimzungumzia Dula Mbabe jana, kocha wake, Omari Perege, alikiri kumpa programu hiyo katika kipindi hiki cha corona.

"Akimaliza kukimbia anarudi nyumbani kwa sababu corona inazidi kushika kasi kila siku kutokana na idadi ya wagonjwa kuongezeka," alisema Perege.

Omari alisema hamruhusu kukaa nje muda mrefu na badala yake amemtaka kuendelea na mazoezi mengine akiwa nyumbani kwake.

Alisema endapo hali ya maambukizi hayo itatulia, Juni mwaka huu bondia huyo anatarajiwa kuelekea nchini Uingereza kucheza pambano la kimataifa.

## Gwambina yataka saba wa kuinogesha Ligi Kuu

**Na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa timu ya Gwambina FC inayoshiriki Ligi Daraja la Kwanza kutoka mkoani Mwanza, umesema unatarajia kusajili wachezaji saba katika mpango wao wa kujiandaa rasmi kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

Akizungumza na Nipashe jana, kutoka mkoani humo kocha mkuu wa timu hiyo, Fulgence Novatus alisema,watasajili wachezaji kutoka katika timu yeyote hapa nchini kwa kuwa wamejipanga kufanya hivyo.

"Tutasajili wachezaji saba ili kupata kikosi kipana ambacho kitaleta ushindani katika Ligi Kuu msimu ujao, alisema Fulgence.

Aliongeza kuwa kwa sasa wanasubiri ligi hiyo kurejea ili wamalizie michezo yao iliyobaki kabla ya kukata tiketi rasmi ya kupanda Ligi Kuu.

"Tunajipanga kuhakikisha tunafanya vizuri katika michezo yetu miwili ili tutimize lengo la kucheza Ligi Kuu," alisema kocha huyo ambaye kikosi chake ni kama kimebakiza tu kukamilisha ratiba ili kupanda Ligi Kuu.

Aidha, alisema kipindi hiki amewapa wachezaji wake programu maalumu ya mazoezi binafsi ambayo wanaendelea kuifanya ili kuiweka sawa miili yao.

Alisema anawasiliana na wachezaji wake mara kwa mara kuhakikisha wanafanya mazoezi kwa umakini mkubwa.

## Corona yatibua soka la ufukweni

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KATIBU wa Kamati ya Soka la Ufukweni wa Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), Khalfan Ali Mohmed, amesema kutokana na mlipuko wa virusi vya corona (COVID-19), vilivyosababisha shughuli zote za michezo kusimama kwa kipindi kisichojulikana, itakuwa ni vigumu kufuata kalenda yao kwa asilimia 100.

Akizungumza na gazeti hili jana, alisema sasa watalazimika kutazama kwanza mfumo wa Shirikisho la Soka duniani (Fifa) na lile la Afrika (Caf), watakaoelekeza juu ya muendelezo wa msimu huu kuhusu soka hilo pindi maambukizi ya virusi vya corona yatakapotulia.

Alisema katika kalenda yao ya kuendesha michuano ya soka hilo, kulikuwa na mambo mbalimbali ikiwamo michuno ya Kombe la Mapinduzi ambayo tayari ilishafanyika, Ligi Kuu ya Zanzibar pamoja na kuanzisha Ligi za Hoteli ili kuhamasiha mchezo huo katika maeneo mbalimbali ya visiwa vya Zanzibar kutokana na kuzungukwa na fukwe kila eneo.

Alisema pia katika kalenda hiyo, ilitakiwa wafanye mafunzo kwa makocha na waamuzi wa soka hilo la ufukweni ili kuwajengea uwezo zaidi katika kufanya shughuli zao hizo na kuwapa elimu ambayo wanaweza kuitoa kwa wengine watakaovutiwa na mchezo huo.

Alisema kutokana na dunia kukumbwa na janga hilo, hatma ya kukamilisha kalenda hiyo sasa itawabidi kuangalia kwanza mashirikisho hayo makubwa.

Michezo

Ijumaa Aprili 24, 2020

Nipashe

HABARI UK.22



## Neymar si kiongozi - Rafael

TIZI POPOTE ...



Nyota wa Juventus, Cristiano Ronaldo, akifanya mazoezi binafsi nyumbani kwake Ureno wakati huu ambao klabu yake imesitisha mazoezi ya pamoja nchini Italia kutokana na mlipuko wa maambukizo ya virusi vya corona vinavyosababisha ugonjwa wa COVID-19. **PICHA MTANDAO**

## Klopp awaonya wapinzani EPL



**LIVERPOOL, England**

JURGEN Klopp ametuma salamu kwa wapinzani wao kwa kusisitiza Liverpool "hawajamaliza kurasa" na bado wanaweza kuwa bora...

## Corona yamtibulia Mbappe usajili Real



**PARIS, Ufaransa**

KYLIAN Mbappe angeuzwa kwa thamani ya euro milioni 300 na alikuwa anakaribia kujiunga na Real Madrid mwaka huu, lakini mlipuko wa virusi vya corona umetibua dili hilo, kwa mujibu wa wakala ambaye amekuwa akifanya kazi mara kwa mara na klabu hiyo ya...

**UK. 21**

# YANGA SASA KIMYA KIMYA

## Yataka kukwepa hujuma katika mchakato wa usajili, yatangaza mapambano...

**Na Somoe Ng'itu**

KUELEKEA msimu mpya, uongozi wa Yanga ya jijini Dar es Salaam, umesema wameongeza umakini katika mchakato wa usajili na sasa wataufanya kimya kimya kwa sababu wanataka kukamilisha mipango yao yote waliyoiweka.

Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Frederick Mwakalebela, aliliambia gazeti hili kuwa, klabu yake imepanga kutorudia makosa ya kuweka wazi majina ya wachezaji inaowahitaji ili kuepuka 'kuhujumiwa'.

Mwakalebela alisema uamuzi huo umewekwa ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

**"Tunajipanga kimya kimya, tutasajili kimya kimya, tunajua lolote linaweza kutokea ndani au nje yetu , hatutaki kuharibu mipango yetu," alisema Mwakalebela.**

Aliongeza pia wanaendelea kuwasiliana na wachezaji wao kwa ajili ya kulinda viwango vyao kwa sababu bado wanaamini wana deni la kumaliza mechi za msimu huu.

"Tunasubiri mwongozo, lakini ni lazima tuwe tayari kwa lolote, la kwanza ni kwamba msimu haujamalizika, hivyo wachezaji lazima wawe tayari kumalizia mechi zilizobakia, benchi la ufundi linasimamia vema na ninaamini hakuna aliyebweteka," aliongeza.

Alisema bado Yanga itaendelea kupambana kuhakikisha inafanya vizuri katika mechi zilizosalia za msimu huu, endapo ligi hiyo itarejea tena.

"Pia tukumbuke kuna mashindano ya Kombe la FA, naamini utaratibu mwingine utatolewa ili kumaliza mashindano hayo, kwetu tutapambana na nafasi ya kushinda taji hili tunayo," Mwakalebela alisema.

Hadi ligi inasimama, Simba ndio walikuwa vinara katika msimamo wa Ligi Kuu Bara, lakini watani hao wa jadi wote wakiwa kwenye hatua ya robo fainali ya michuano ya Kombe la FA ambayo bingwa wake hukata tiketi ya kushiriki mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

770856 541002 >